# ATHARI ZA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO KWA NYIMBO ZA WATOTO WAISHIO MIJINI

**Na**

**Bimkubwa Abdulrahman Hemed**

**Tasnifu kwa Ajili ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Cha Dodoma**

**Chuo Kikuu cha Dodoma**

**Oktoba, 2015**

# ITHIBATI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma na amependekeza tasnifu hii inayoitwa **“Athari za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Nyimbo za Watoto waishio Mjini Zanzibar”**, amependekeza ikubaliwe kwa minajili ya kutunukiwa shahada ya uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

……………………………………………….

Dkt. Elias Manandi Songoyi

(Msimamizi)

Tarehe……………………………

## IKIRARI NA HAKI MILIKI

Mimi, Bimkubwa Abdulrahman Hemed, ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu asilia, na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kutunukiwa shahada inayofanana na hii au nyingine yoyote.

Saini……………………………………………….

Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ile bila ya kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu au Chuo Kikuu cha Dodoma.

# TABARUKU

Kwa mama yangu mpenzi Biima Nassor Hemed, watoto wangu Lujayna na Irfaan na mume wangu mpenzi Rashad Said Ali. Mungu awalinde na shari za dunia na akhera na awalipe malipo mema.

## SHUKURANI

Kwanza namshukuru Allah Subhanahu Wataala kwa kuniwezesha kufanya utafiti huu na kuukamilisha nikiwa ni mzima wa afya. Bila ya uwezo wake nisingefanikiwa na jambo lolote.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitomshukuru mwalimu wangu na msimamizi wangu wa utafiti huu Dkt Elias Manandi Songoyi ambaye kwa miongozo yake na ushirikiano ameniwezesha kufanya utafiti huu hadi kukamilika. Mungu akulipe kheri daima. Pia, namshukuru Dkt Rafiki Y. Sebonde kwa muongozo wake katika somo la utafiti na mbinu zake na Dkt Athuman Ponera kwa kutupa taaluma ya ziada na kutuongoza vyema katika uwandishi wa utafiti. Allah akujaze khayraat. Maelekezo ya wote hawa yalikuwa ni muhimu katika kufanikisha utafiti huu.

Vile vile, shukrani zangu za dhati zimwendee Rashad Said Ali, Biima Nassor, Dkt Maulid Haji Omar wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Lujayna na Irfaan kwa uvumilivu wao na ustahamilivu wao katika kipindi chote hiki kigumu hadi kumalizika kwa kazi hii.

Nakamilisha shukran zangu kwa wanafunzi wote wa Chuo Kikuu cha Dodoma hususan, Abdi Ramadhan Mberwa kwa kuwa pamoja katika kipindi chote hiki kigumu hadi kukamilisha utafiti huu Allah amfanyie wepesi katika mambo yake na amzidishie baraka. Pamoja na wale wote ambao wametoa mchango wa hali na mali katika kukamilisha kazi hii, nawambia ahsanteni Allah awazidishie Baraka Amiyn.

# IKISIRI

Utafiti huu umechunguza namna Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inavyoathiri nyimbo za watoto hususan maeneo ya mijini ambako maendeleo hayo ya sayansi na teknolojia ndiko yanakopatikana kwa wingi.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Usosholojia iliyoasisiwa kwa kuja kupingana na ulimbwende karne ya kumi na tisa. Utafiti huu umejumuisha mbinu ya mahojiano na hojaji kukusanya data hatimaye imechanganuliwa kwa njia ya maelezo.

Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano yaliyopo nchini hususan mijini, yameathiri kwa kiasi kikubwa nyimbo za watoto kutokana na kuwepo kwa vyombo vingi vya habari hapa nchini, ambao ushindani wao wa kibiashara ndio unaowafanya warushe hewani nyimbo za wasanii mbali mbali na kuacha zile za watoto ambapo watoto walikuwa wanaziimba kabla yake.

Suala la msingi lililobainishwa na utafiti huu ni kwamba nyimbo za watoto zimeathiriwa na maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, mapendekezo yafuatayo yamezingatiwa. Serikali na jamii wafanye juhudi za makusudi kurejesha hadhi ya nyimbo za watoto kwa kuziingiza katika mitaala ya shule pamoja na wazazi kufanya juhudi za makusudi kuwafundisha nyimbo hizo ili zisiendelee kupotea. Pia, imependekezwa tafiti zaidi zifanywe kuhusu tanzu mbalimbali za fasihi simulizi, na kwamba watafiti wasikidharau kipengele hiki cha nyimbo za watoto kwani mbali na kutoa burudani, pia watoto hupata mazoezi ya kutosha nakuwafanya wawe wakakamavu na wenye afya.

## YALIYOMO

ITHIBATI ........................................................................................................i
IKIRARI NA HAKI MILIKI ..........................................................................ii
TABARUKU ................................................................................................ iii
SHUKURANI ..............................................................................................iv
IKISIRI..........................................................................................................v
YALIYOMO ..................................................................................................vi

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ........................................................1**
1.0 Utangulizi ...................................................................................................1
1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti ..........................................................................1
1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti ..........................................................................3
1.3Malengo ya Utafiti ......................................................................................3
1.3.1 Lengo la Jumla .........................................................................................3
1.3.2 Malengo Mahsusi ......................................................................................3
1.4 Maswali ya Utafiti ......................................................................................3
1.5 Umuhimu wa Utafiti ...................................................................................4
1.6 Kiunzi cha Nadharia ....................................................................................4
1.7 Changamoto katika Utafiti ..........................................................................5
1.8 Hitimisho ....................................................................................................6

**SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO.............................................7**
2.0 Utangulizi ...................................................................................................7
2.1 Nyimbo za Watoto kwa Ujumla ..................................................................7
2.1.1 Fasili za Nyimbo za Watoto .....................................................................7
2.1.2 Fani, Maudhui na Dhima za Nyimbo za Watoto ......................................10
2.2 Sayansi na Teknolojia na Nyimbo za Watoto ............................................13
2.3 Mapengo Yaliyojitokeza ............................................................................15
2.4 Hitimisho ....................................................................................................15

**SURA YA TATU: MBINU NA ZANA ZA UTAFITI ..................................16**
3.0 Utangulizi ...................................................................................................16
3.1 Mpango wa Utafiti .......................................................................................16

3.2 Eneo la Utafiti ........................................................................................16
3.3 Walengwa wa Utafiti ...................................................................................17
3.3.1 Sampuli .....................................................................................................17
3.4 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ....................................................................18
3.4.1 Mbinu ya Usaili........................................................................................19
3.4.2 Ushuhudiaji ..............................................................................................19
3.4.3 Udurusu wa Maktaba ...............................................................................19
3.5 Ukusanyaji wa Data ....................................................................................20
3.5.1 Zana za Kukusanyia Data ........................................................................20
3.5.1.1 Daftari la Kumbukumbu na Kalamu......................................................20
3.5.1.2 Kinasa Sauti ..........................................................................................20
3.5.1.3 Simu ya Kiganjani..................................................................................21
3.5.1.4 Kompyuta...............................................................................................21
3.6 Ufaafu na Udhibiti wa Data ........................................................................21
3.7 Masuala ya Maadili ya Utafiti.....................................................................21
3.8 Uchambuzi na Uunganishwaji wa Data ......................................................21
3.9 Mipaka ya Utafiti ........................................................................................22
3.10 Hitimisho...................................................................................................22

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI WA DATA NA MJADALA WA MATOKEO. ........................................................................................23**
4.0 Utangulizi....................................................................................................23
4.1 Uwasilishaji, Uchambuzi wa Data na Mjadala wa Matokeo .......................23
4.1.2.1 Historia ya Nyimbo za Watoto Kabla na Baada ya Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia ..........................................................................................30
4.1.2.2 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Uwasilishaji.............................34
4.1.2.3 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Dhima......................................46
4.1.2.3 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Uhifadhi ..................................55
4.1.3 Mchango wa Sayansi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Nyimbo za Watoto Waishio Mjini Zanzibar ..............................................................57
4.1.3.1 Uwasilishaji............................................................................................57
4.1.3.2 Dhima.....................................................................................................60

4.1.3.3 Uhifadhi ........................................................................................................61
4.2 Hitimisho..................................................................................................................62

**SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO........................................64**
5.1 Utangulizi...................................................................................................................64
5.2 Hitimisho...................................................................................................................64
5.3 Mapendekezo ...........................................................................................................65
5.4 Hitimisho...................................................................................................................66
**MAREJELEO .........................................................................................................67**
**VIAMBATISHO .....................................................................................................69**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii ni utangulizi unaoelezea mpango na mchakato wa utafiti huu na ina vipengele vinavyoeleza usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, kiunzi cha nadharia, changamoto katika utafiti na hitimisho.

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Historia inaeleza kuwa mara tu baaada ya binaadamu kuanza kuishi pamoja, ilizuka haja ya mawasiliano ambayo yaliibua fasihi, ambayo jamii inaitumia katika kuelekezana vipengele mbalimbali vinavyohusu maisha kwa jumla. TAKILUKI (1982) wanasema kuwa kila jamii ina fasihi yake. Wazanzibari, kama jamii nyingine, wana fasihi yao ambayo huitumia katika kueleweshana vipengele mbalimbali vya kimaisha kama vile, kimapenzi, kisiasa, kiuchumi, kidini na kimaadili.

Fasihi ni sanaa itumiayo maneno ili kutoa picha ya mwanadamu akiwa maishani mwake, mahusiano yake na viumbe wengine, migogoro yake na mazingira, shida zake, raha zake, matumaini yake na jinsi anavyopiga hatua katika maendeleo yake.

Kabla ya kukua kwa maendeleo ya habari na mawasiliano katika jamii ya Tanzania Zanzibar, nyimbo za watoto zilikuwa zikitolewa au kuwasilishwa kwa njia ya mdomo na papo kwa papo. Fanani na hadhira ilikuwa ikikaa pamoja. Hivyo, jamii ili kuweza kusikia wimbo wowote ilikuwa ni lazima mwimbaji awe pamoja na hadhira yake. Ikiwa msanii au mwimbaji wa wimbo hayupo, hivyo basi hadhira haiwezi kuusikia wimbo huo na ikiwa msanii huyo amefariki wimbo huo utakuwa ni mali ya

jamii na hauna mmiliki binafsi au wakati mwengine kutoweka kutokana na kuhifadhiwa kichwani.

Nyimbo zote walizokuwa wakiziimba watoto zikihifadhiwa vichwani mwao, na zilikuwa zikisambazwa kwa kutumia njia ya mdomo pekee.

Kutokana na kukua na kuenea kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, nyimbo za watoto waishio mjini zimebadilika sana katika uwasilishwaji wake ikilinganishwa na nyimbo ambazo watoto walikuwa wakiziimba kabla ya kukua na kuendelea kwa teknolojia ya habari na mawasiliano katika uwasilishaji na usambazaji wake. Hii inatokana na mabadiliko ya ulimwengu ya kuitaka dunia yote iwe kama kijiji kimawasiliano.

Siku hizi kutokana na maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano, watoto wengi waishio mijini wamekuwa wakiimba nyimbo zao ambazo zimeathiriwa na nyimbo za wasanii mbalimbali ambazo zimeenea kutokana na kuwepo kwa vyombo vya habari na mawasiliano maeneo ya mijini.

Radio, runinga, magazeti, video na Intaneti, vimeathiri sana nyimbo za watoto katika uwasilishwaji wake na utendaji wake, usambazaji wake pamoja na matini za nyimbo hizo. Katika uwasilishaji wa nyimbo kwa kutumia vyombo hivi, mwimbaji au mtunzi wa nyimbo, si lazima awepo katika mazingira ambayo hadhira ipo kutokana na nyimbo hizo kuhifadhiwa na kusambazwa kupitia vyombo hivyo.

Kutokana na sababu hizo, mtafiti ameona kuwa ipo haja ya kuchunguza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano pamoja na athari zake kwa nyimbo za watoto waishio mijini Zanzibar.

## 1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Kabla ya maendeleo ya habari na mawasilano katika jamii, katika jamii nyimbo za watoto zilikuwa zikiimbwa kwa njia ya mdomo. Baada ya kuibuka kwa sayansi na teknolojia, mabadiliko makubwa katika nyanja mbalimbali za kimaisha, hata nyimbo za watoto, yalitokea hasa katika uwasilishaji wake. Kutokana na hali hiyo, kumekuwa na haja ya kufanya utafiti kuona ni kwa jinsi gani maendeleo hayo yameathiri nyimbo za watoto. Utafiti huu ni moja ya jitihada zinazofanywa na wataalam mbalimbali kulichunguza swali hili.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

### 1.3.1 Lengo la Jumla

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza na kubainisha athari za teknolojia ya habari na mawasiliano kwa nyimbo za watoto waishio mjini Zanzibar.

### 1.3.2 Malengo Mahsusi

i. Kubainisha athari za maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa nyimbo za watoto katika uwasilishaji na dhima.

ii. Kubainisha mchango wa maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika maendeleo ya fasihi simulizi katika utanzu wa nyimbo za watoto, mjini Zanzibar.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

i. Ni kwa namna gani dhima ya nyimbo za watoto wa Zanzibar Mjini na uwasilishaji wake zimeathiriwa na maendeleo ya TEHAMA?

ii. Pamoja na athari hizo, nini mchango wa maendeleo ya TEHAMA katika maendeleo ya nyimbo za watoto wa mjini Zanzibar?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utawasaidia walimu na wanafunzi wa fasihi katika kuibua dhima, uwasilishaji na uhifadhi wa nyimbo za watoto katika maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano**.** Pia, utawafaidisha wanafasihi wa taaluma ya fasihi kupata marejeleo na muongozo mzuri wa tafiti zao. Aidha, utafiti huu utawasaidia watoto wa rika zote, wazee, watafiti, Serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali, kwa kupata nguvu kazi imara itakayosaidia kuleta maendeleo katika jamii.

## 1.6 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Sosholojia katika uchambuzi na uchanganuzi wa data. Nadharia ya Sosholojia ni nadharia inayohusishwa na mtaalam wa Kifaransa Hippolyte Taine katika karne ya 19. Hapo kabla ilidhaniwa kwamba iko nje ya muktadha lakini ilikisudiwa kutumika katika karne ya 20 ya fasihi. Kwa hivyo, nadharia hii ilipata mashiko na ilijulikana zaidi na waandishi wa fasihi wa karne ya 20 hususan maeneo ya Afrika.

Nadharia ya Sosholojia ilibuka kutokana na kuanguka kwa uchumi ulioikumba bara la Ulaya. Hali hiyo ilisababisha kutokea kwa uhaba wa bidhaa. Kuanguka kwa uchumi kuliwafanya watu waanze kufikiria mbinu za kulitatua tatizo hilo. Katika mchakato wa kulijadili na kulitafutia ufumbuzi sakata la uchumi duni, wataalam wa fasihi walichukuwa nafasi ya kuwa kama ni walimu na washauri kwa kufikisha mawazo yao kwa kupitia fasihi. Kutokana na kwamba nadharia hii inashughulikia mambo ya kijamii, wanafasihi wanapotunga kazi zao huwa hawaoti bali huangalia jamii ina matatizo gani na inahitaji nini kwa muda gani. Hivyo, mara nyingi jamii hukumbwa na mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Fasihi inayofuata nadharia ya kisosholojia huambatana na mabadiliko hayo. Fasihi hiyo

huwa ni kioo cha jamii husika, ndani ya fasihi ndimo watu wanamopata ujasiri wa kudai uhuru, haki na kupata nguvu za kuungana pamoja ili kufikia malengo waliyoyakusudia kwa kusoma vitabu mbalimbali vya wanafasihi pamoja na kuangalia au kusikiliza tamthilia mbalimbali kupitia vyombo vya habari. Fasihi simulizi imekumbwa na mabadiliko hayo kupitia uwasilishaji wake na hata uhifadhi wa fasihi hiyo. Nyimbo za watoto ni miongoni mwa fasihi simulizi ambayo ni zao la jamii, fasihi ambayo imekumbwa na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Muhimili mkubwa wa nadharia hii ni fasihi na jamii. Hivyo, nadharia hii ya kisosholojia imemsaidia sana mtafiti kupata data za uhakika ambazo ndio kusudio la mtafiti kuangalia mabadiliko hayo ya fasihi katika jamii ambayo huchangiwa na mambo tofauti yanayojitokeza katika jamii zote duniani. Hivyo, mabadiliko ya nyimbo za watoto wa mjini ni zao la nadharia hii ya kijamii, kwani fasihi ianayotumia nadharia hii huzaliwa, hukua na hufa kama ilivyo kwa jamii yenyewe.

**1.7 Changamoto katika Utafiti**

Kuna vikwazo mbalimbali vilivyoweza kujitokeza katika zoezi zima la utafiti huu ikiwa ni pamoja na kukosa ushirikiano wa moja kwa moja kwa baadhi ya watoto, wazazi na walezi.Tatizo hili lilitokana na sababu kuwa wengi wa wazazi na walezi hawana uelewa zaidi wa umuhimu wa kufanya utafiti. Hivyo, tatizo hili lilikwaza kuzipata data kwa uharaka.

Mtafiti alichukua juhudi za makusudi za kuwaelimisha wazazi na walezi na hatimaye kupata ushirikiano mzuri.

Pia, tatizo jengine lililojitokeza katika zoezi zima la ukusanyaji wa data za utafiti huu ni mabadiliko ya hali ya hewa, kwani pindi data zilipokuwa zinakusanywa na

mtafiti kulikuwa na mvua ambayo ilisababisha kubadilika kwa ratiba zilizotumika katika kuukamilisha utafiti huu.

Vile vile, ufungwaji wa skuli ni tatizo lililozorotesha ukusanyaji wa data za utafiti huu, kwani kipindi cha ukusanyaji wa data, skuli zilikuwa zimefungwa kwa ajili ya mitihani ya kidato cha nne, cha pili na darasa la saba.

Hata hivyo, mtafiti aliweza kujitahidi kuwaelimisha baadhi ya walezi na wazazi umuhimu wa utafiti huu, baadhi yao waliweza kuelewa na kutoa mchango pale walipoweza na kusaidia kufanikisha data hizo.

## 1.8 Hitimisho

Katika sura hii ya utangulizi, vipengele mbalimbali vimezungumziwa ambavyo vinatoa mwongozo na mwelekeo wa utafiti huu. Vipengele hivyo ni usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, kiunzi cha nadharia na changamoto katika utafiti. Sura inayofuata itaelezea mapitio ya maandiko ya kazi mbalimbali yaliyohusiana na utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imeangalia kazi mbalimbali ambazo zimefanywa na wataalam wa fasihi katika uwanja wa nyimbo za watoto. Sura hii imegawanyika kwa kuangalia mapitio yanayohusu nyimbo za watoto kwa ujumla, fasili ya nyimbo za watoto, fani, maudhui na dhima za nyimbo za watoto, sayansi na teknolojia na nyimbo za watoto, mapengo yaliyojitokeza na hitimisho.

## 2.1 Nyimbo za Watoto kwa Ujumla

Nyimbo za watoto ni miongoni mwa utanzu mkongwe wa fasihi simulizi, ambao umekusudiwa kuwaburudisha, kuwaelimisha na kuwa ni sehemu ya kujenga afya za watoto kimwili na kiakili, kwani ndani yake kuna mazoezi tosha ambayo huwafanya watoto wachangamke wakati wa kuimba na kucheza.

### 2.1.1 Fasili za Nyimbo za Watoto

Katika kipengele hiki kimeeleza maana mbalimbali zinazohusu na nyimbo za watoto pamoja na baadhi ya istilahi maalumu ambazo zimetumika katika mada ya utafiti huu.

**Sayansi na Teknolojia** ni dhana zinazohusiana sana. Hivyo, inapozungumziwa teknolojia huwa na maana ya maendeleo ya juu zaidi ya kisayansi. Kwa hivyo basi, Sayansi na Teknolojia ni vitu viwili vinavyokwenda sambamba bila kuachana.Teknolojia ni maendeleo ya kisayansi katika hatua ya mwisho kabisa ambayo inaonekana. Kwa mujibu wa (sw Wikipedia.org/wiki/sayansi) wamefafanua kuwa; **Sayansi** ni maarifa yanayopatikana kwa kufanya vitendo, kutazama na

kujaribu kweli zilizobainishwa pasi na kuthibitishwa. Sayansi ilianza kama udadisi wa mtu mmoja tu; lakini kadri mawazo yanapotanuka, inakuwa vigumu kwa mtu mmoja kufanya mchango wa kujitenga, kwa hivyo, jumuiya zimebeba kusudi ambalo hapo mwanzo ilionekana kama ni shauku ya mtu mmoja mmoja kama awali.

**Sayansi na jamii** huenda pamoja katika kuleta mabadiliko, kwa vile mabadiliko huletwa na watu wenyewe.

Kadeghe, (2000), anasema sayansi ni elimu ambayo mtu huipata kwa kufuata taratibu za kisayansi katika kufikia jibu au kutoa hitimisho. Mara nyingi elimu hii hupatikana kwa kufanya uchunguzi na ugunduzi, Mwanasayansi ni mtu yoyote anaejishughulisha na upatikanaji wa elimu maarifa kwa kufuata taratibu zenye njia maalum za kisayansi.

Maendeleo hayo ya Sayansi na Teknolojia ndiyo yaliyohusishwa na kukua na kuenea kwa vyombo mbalimbali vya habari na mawasiliano ambavyo ni radio, televisheni, video na intaneti ambavyo vimeathiri nyimbo za watoto waishio maeneo ya mijini.

Hivyo basi, dhana ya teknolojia imefasiliwa kutoka dhana ya sayansi. Istilahi teknolojia, katika lugha ya Kiswahili imetoholewa kutoka neno “Technology”. Istilahi hii katika lugha ya Kiswahili imeenea zaidi kutokana na kukua na kuenea kwa utandawazi duniani.

> Wamitila K.W. (2003), katika kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia anasema;
> “Utandawazi ni dhana inayotumiwa kueleza mikabala ya kiutamaduni, kiuchumi na hata kisiasa ambayo inasisitiza muungano na mahusiano yanayokiuka mipaka ya taifa –dola. Mikabala hii inatambulishwa na kupungua kwa uwezo wa mataifa –dola wa kuyadhibiti matukio hata katika maeneo au nchi zao wenyewe

> huhusisha pia kazi za kimazingira au kiutamaduni (kwa mfano kuenea na kusambaa kwa tamaduni za kila aina kutoka sehemu moja hadi nyingine na kuathiri suala la UJITAMBUZI. Mtazamo wa utandawazi unatazamwa kama unaaathiri mataifa ya kimaskini vibaya kwa kuwa yanalazimishwa kupambana na kushindana na mataifa makubwa ya kimataifa."

Baadhi ya watafitiwa wameeleza kuwa kukua na kuenea kwa teknolojia ya habari na mawasiliano katika maeneo ya mijini nchini Tanzania, kumesababisha kuenea kwa vyombo mbalimbali vya habari na mawasiliano ambavyo vimeleta athari katika nyimbo wanazoziimba watoto. Watoto ni wepesi sana kujifunza na kuweza kutumia vifaa hivi vya teknolojia ya habari na mawasiliano, na wengi wa watoto waishio mijini hawana ufahamu na ujuzi wa kuchuja faida ya vyombo hivyo na athari zake. Aidha, wamefafanua kwamba mara nyingi watoto huiga mawazo na mitindo ya nyimbo waipatayo kupitia vyombo hivyo, pasipo kuchuja ubora na athari zake katika nyimbo waziimbazo pamoja na michezo yao.

Vile vile, wadau wa habari ambao mtafiti amepata bahati ya kuwahoji wamedai kuwa, maendeleo ya Teknolojia ya habari na mawasiliano yameigeuza dunia kuonekana kama kijiji na kufanya muingiliano wa tamaduni za jamii mbalimbali kuwa pamoja. Udogo huu wa dunia kuwa kama kijiji, ndio ambao umesababisha kujitokeza kwa athari nyingi katika nyimbo za watoto waishio mijini.Wadau hao wametumia kigezo cha Mtaalamu wa mawasiliano Marshall, (2003:108), kwa kumnukuu anavyosema kuwa;

> "Dunia inabadilika na kuwa ndogo kila kukicha, na matokeo yake ni kuzaliwa mawasiliano ya kisasa duniani. Hali hii inasababisha kuzaliwa kwa dhana ya teknolojia mpya".

Maendeleo hayo ndiyo yaliyosababisha kukua na kuenea kwa vyombo mbalimbali vya habari na mawasiliano ambavyo vimeleta athari katika nyimbo zinazoimbwa na

watoto. Kutokana na ukuaji huu wa Teknolojia ya habari, kuathirika kwa nyimbo za watoto ni jambo lisiloepukika kwa sababu ya maendeleo hayo kuenea zaidi katika jamii, zaidi maeneo ya mijini ambako vyombo hivyo vya habari na mawasiliano hupatikana kwa wingi na kwa urahisi na kuenea zaidi kutokana na jamii kuathiriwa sana na teknolojia hiyo.

### 2.1.2 Fani, Maudhui na Dhima za Nyimbo za Watoto

Finnegan (1992), ameeleza kuwa nyimbo za watoto hapo zamani zilikuwa zinawasilishwa kwa njia ya masimulizi au ya mdomo kwa maana nyingine. Kwa wakati huo njia hii ilikuwa ni bora kwani ilikuwa inawafundisha watoto maadili ya jamii, kwani hakukuwa na kitu kingine ambacho watoto walikuwa wanakipata kama mafundisho. Jamii ya wakati ule ilikuwa inakaa karibu sana na watoto kuwafundisha maadili kupitia fasihi simulizi hususan, nyakati za usiku. Mabibi na mababu walikuwa wakitumia fursa hiyo kuwaelimisha watoto na wajukuu zao mambo mbalimbali yaliyomo katika jamii na namna ya kukabiliana nayo. Baadaye, njia hii ilionekana kupoteza muelekeo na kusaidia kufa kwa fasihi hiyo kwani wale wazee ambao ndio tegemeo la kuirithisha fasihi hii kufa, hivyo kuonekana kwamba fasihi nayo ianaweza kupotea.  Changamoto hiyo ndiyo iliyomfanya Finnegan afanye utafiti wa kina kuhusiana na uhifadhi wa fasihi simulizi alioufanya katika Chuo Kikuu cha London aliona ipo haja sasa ya fasihi hii kuhifadhiwa kupitia njia mbalimbali za uhifadhi kama vile maandishi na uhifadhi mwingine. Mchango wa Finnegan umetoa mwanga katika mchakato wa kuipata mada kwani nyimbo za watoto za miaka hii zimekuwa na tofauti kubwa katika uwasilishaji, dhima na uhifadhi ambapo jambo hili, mtaalamu huyu ameshalizungumzia. Athari ya fasihi simulizi kuhifadhiwa vifuani mwa watu inaweza kupotea baada ya kufa kwa mtu

aliyehifadhi, lakini iwapo itahifadhiwa kwa njia za kisasa inaweza kudumu kwa muda mrefu.

Simiyu (2002), ameeleza kuwa nyimbo za watoto ni aina ya nyimbo ambazo huimbwa au huimbiwa watoto ili washawishike kihisia kufanya jambo fulani kama vile kulala au kunyamaza. Katika utafiti wake amezungumzia mandhari yanayotumika katika nyimbo za watoto pamoja na wakati wa kuzitumia nyimbo hizo kwa kutoa mifano mbalimbali ya nyimbo kama vile nyimbo za chekechea, nyimbo za michezo, na nyimbo bembelezi. Maelezo haya yamechangia katika kuelewa maana ya dhana hii: nyimbo za watoto kwa ujumla wake.

Nyimbo za watoto zikiwa ni sehemu ya fasihi simulizi, katika enzi hizi, husikika radioni na huonyeshwa kwenye televisheni kwenye vipindi mbalimbali zikiwa zinaghaniwa na watoto. Pia, nyimbo nyingi husikika zikiwa zinaimbwa na watoto wawapo katika michezo yao; kwa mfano nyimbo nyingi huimbwa na watoto katika vipindi vinavyorushwa hewani na vyombo vya habari, radio na televisheni. Wataalamu wengi wameweza kuchunguza na kujadili nyimbo hizo.

Opie na Opie, (1977) wanadai kuwa nyimbo za watoto zimegawanyika katika makundi mbali mbali yenye kuzitofautisha. Kuna baadhi ya nyimbo ambazo huimbwa na watoto walizofundishwa na watu wazima katika jamii waishimo. Nyimbo hizo zote kwa ujumla huweza kuakisi utamaduni wa jamii husika wenye kufuatwa na jamii hiyo, ijapokuwa baadhi ya nyimbo hizo huwa na maudhui yake yenye kuwahusu watoto wa jamii hiyo.

Mbarouk, (1983), ameeleza vizuri umuhimu wa nyimbo za watoto waziimbazo katika michezo yao, moja ya dhima ya nyimbo hizo ni liwazo. Akitoa mfano wa

nyimbo ya “Kachiri” unaoimbwa na watoto wa Kizanzibari, Mbarouk anaeleza kwamba wimbo huu humfundisha mtoto wa kike kuvumilia shida pindi anapoolewa na mumewe kupata safari. Wimbo huu huimbwa na watoto wa kike wanapocheza.

Kachiriii iii kachiri saga
Mume wangu kasafiri saga
Kaniachia ukili saga
Na kipande cha Hariri………………….

Aidha, ameufafanua wimbo huu kwamba, huimbwa na watoto wa kike wakiwa katika michezo yao, huku wakisaga saga miguu yao chini. Maudhui ya wimbo huu ni kumburudisha na kumuelimisha mtoto wa kike kuvumilia shida za upweke pindi mumewe anapokuwa safarini. Pia, kujenga afya za miili yao kwani namna ya uchezaji wa wimbo huu ni zoezi tosha ambalo humfanya mtoto ajisikie vizuri baada ya kumaliza kucheza. Hivyo, huwasaidia watoto kujenga ukakamavu na kuwa tayari kukabiliana na matatizo yote yanayoweza kuwakumba pindi wakiwa peke yao. Nyimbo nyingi za watoto hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Tofauti hizo hutokana na tofauti ya mazingira, ijapokuwa kuna baadhi ya nyimbo zenye kubeba maudhui yenye kufanana katika jamii mbali mbali.

Mdowe (2011), amezungumzia nyimbo za watoto zinavyobadilika na wakati kifani na kimaudhui katika Wilaya ya Magharibi Unguja. Katika utafiti wake amegusia jinsi wakati unavyobadilisha muundo, mtindo na maudhui ya nyimbo za watoto. Kipengele cha athari za sayansi na teknolojia ameizungumza kwa kiwango kidogo sana kwa maendeleo ya nyimbo za watoto, alichokijadili sana ni matumizi ya lugha ya picha, ishara pamoja na mabadiliko ya uwasilishaji yanavyochangia kuibua maudhui katika nyimbo za watoto. Kwa hivyo, utafiti huu umetoa mchango mkubwa hasa katika kipengele cha uwasilishaji na dhima ambavyo vimejadiliwa.

Haji na wenzake, (1983), wamechambua kwa mifano nyimbo mbalimbali za watoto wa Kizanzibari na kuelezea baadhi ya michezo inayochezwa katika nyimbo hizo. Wameeleza kuwa, baadhi ya nyimbo za watoto zina maana kamili na hutoa mafunzo fulani, katika maelezo yao wamesema, michezo ya watoto ya Zanzibar hutofautiana kulingana na mazingira, wakati, mila na utamaduni. Kwa mfano, wameeleza kuwa wakati mwingine nyimbo za watoto waishio Unguja hutofautiana na wa kisiwa cha Pemba. Ingawa, mara nyingine kwa baadhi ya michezo hufanana na kutofautiana kwa kiwango kidogo. Wataalamu hawa wamemsaidia mtafiti kuzisoma nyimbo mbalimbali za kiasili walizokuwa wakiimba watoto katika mazingira ya kawaida na kupata kufahamu ni namna gani watoto wa sehemu tofauti wanaimba nyimbo zao ambazo zina ladha moja ambayo hutofautishwa na mazingira tu.

## 2.2 Sayansi na Teknolojia na Nyimbo za Watoto

Maendeleo ya Teknolojia ya habari na mawasiliano ambayo ni matokeo ya kukua na kuenea kwa sayansi na teknolojia duniani katika karne hii ya ishirini na moja, yameathiri sana nyimbo za watoto waishio mijini. Maendeleo hayo ya sayansi na teknolojia ndiyo yaliyosababisha kutokea na kuenea kwa vyombo vya habari na mawasiliano.

Nyimbo nyingi za watoto waishio mijini zimeathiriwa na maendeleo haya kutokana na ugumu wa kuyaepuka na athari zake kwa fasihi kwa ujumla ni kubwa.

Kezilahabi anasema;

> Fasihi imo katika karne ya Sayansi na Teknolojia lazima ijieleze katika mazingira hayo na kukua kwake hakuwezi kutenganishwa na teknolojia ya neno…Tusione teknolojia kama kitu huria ambacho hutegemea tu mtunzi Teknolojia ndiyo inayokata shauri juu ya mwelekeo wa kibinaadamu ingawaje tunaigundua wenyewe.
>
> (Kezilahabi, 1995:14)

Nyimbo za watoto ni miongoni mwa tanzu za fasihi simulizi ambazo zimeathiriwa sana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Hivyo basi, maendeleo hayo ya sayansi na teknolojia, hususan TEHAMA, yamechangia sana katika maendeleo ya kukua kwa nyimbo ziimbwazo na wasanii wa muziki wa kizazi kipya hapa Tanzania na, kwa namna moja au nyengine huathiri nyimbo za watoto waishio mijini.

Materu, (1983), ameeleza dhana ya fasihi simulizi na uwandishi wa kiswahili katika fasihi. Aidha, amejadili mchango wa sayansi ya uandishi wa fasihi simulizi na kubainisha athari namchango wake. Materu ameonesha ni kwa kiasi gani fasihi simulizi ilivyokuwa ikiwasilishwa kwa hadhira na mabadiliko yake mara baada ya kuibuka kwa maandishi. Kwa hivyo, ingawaje amezungumzia fasihi simulizi kwa ujumla lakini kazi yake imetoa muongozo mzuri katika kubaini baadhi ya athari za sayansi ya habari na mawasiliano katika nyimbo za watoto.

Kitundu (2011), amejadili athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia kwenye fasihi simulizi kwa kutumia kipengele cha nyimbo za ibada za dini ya Kikristo. Katika utafiti wake, amejadili historia ya uimbaji wa nyimbo za ibada kabla ya maendeleo ya habari na mawasiliano nchini Tanzania. Vile vile, amebainisha athari za maendeleo za teknolojia katika nyimbo hizo katika utungaji, uwasilishaji, uhifadhi, usambazaji na dhima. Mwisho, akabainisha mchango wa maendeleo ya sayansi na teknolojia katika kuiendeleza fasihi simulizi hususan nyimbo za ibada. Kwa hivyo, ingawa mtaalamu huyu anaonekana wazi kuwa hakuzungumzia hata kidogo nyimbo za watoto, lakini kazi yake imetoa dira kwani nyimbo za Injili na nyimbo za watoto zote hupatikana katika utanzu mmoja wa fasihi simulizi. Hivyo, bila shaka athari zinazopatikana katika nyimbo za Injili inawezekana ikawa ndio

zilezile zinazopatikana katika nyimbo za watoto. Kutokana na muongozo huo mchango wa Kitundu umekuwa muafaka katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data.

## 2.3 Mapengo Yaliyojitokeza

Ingawa tafiti nyingi zinazohusu nyimbo za watoto pamoja na maendeleo ya sayansi na teknolojia zimeshafanywa, lakini bado inaonekana kwamba baadhi ya vipengele katika nyimbo hizo havijagusiwa. Katika udurusu wa mapitio mbalimbali imebainika kuwa athari za maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano halijagusiwa sana hususan Zanzibar. Kwa hiyo, katika utafiti, huu umeonekana ni vyema kuziangalia athari hizo hasa kwa watoto waishio mjini Zanzibar, kwani wao ndio waathirika wakubwa wa maendeleo na mabadiliko ya TEHAMA.

## 2.4 Hitimisho

Sura hii ni mapitio ya maandiko mbalimbali yaliyotumiwa na mtafiti katika kazi hii. Mapitio hayo, yamehusu nyimbo za watoto pamoja na athari na mchango wa maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika fasihi simulizi. Sura ifuatayo itaelezea mbinu na zana za utafiti.

## SURA YA TATU

## MBINU NA ZANA ZA UTAFITI

### 3.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea mchakato wa utafiti, eneo la utafiti na ina vipengele vifuatavyo: Mpango wa utafiti, Eneo la utafiti, Walengwa wa utafiti, Sampuli ya watafitiwa, Mbinu za utafiti, Ukusanyaji wa data, Ufaafu na Udhibiti wa data, Maswala ya maadili ya utafiti, Uchambuzi na Uunganishwaji wa data, Mipaka ya utafiti na Hitimisho.

### 3.1 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu umefanyika maktabani na uwandani. Mtafiti amekusanya data mbalimbali kutoka maktaba zinazohusu nyimbo za watoto kwa ujumla na sayansi na teknolojia. Aidha, mtafiti amesoma baadhi ya kazi za fasihi zinazohusiana na athari za sayansi na teknolojia kwenye fasihi simulizi kwa ujumla na kwenye nyimbo za watoto.

Mbinu ya ufafanuzi na uelezaji wa mambo kwa undani ndiyo iliyotumika zaidi kwa uwasilishaji wa matokeo ya utafiti huu. Data zilizokusanywa zimechambuliwa na kuhakikiwa. Vile vile, mtafiti amekwenda moja kwa moja kwa watoto waishio mijini na kuchunguza jinsi maendeleo ya habari na mawasiliano yalivyoathiri nyimbo hizo.

### 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika Skuli ya Mkunazini na Darajani ambazo zipo Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar. Eneo hilo lipo katikati ya mji wa Zanzibar. Mtafiti amechagua maeneo hayo kwa sababu yamekusanya watoto wengi

ambao tayari wameshaathiriwa na matumizi ya vyombo vya sayansi na teknolojia kama vile simu, luninga na kompyuta. Aidha ni eneo ambalo idadi kubwa ya watoto hujishirikisha katika kuingia katika kumbi za starehe za watoto yaani “Disko Toto”. Kwa hivyo, mtafiti aliweza kupata data za aina tofauti kutokana na vijana wenyewe kuhusuka moja kwa moja katika kushiriki kwenye nyimbo na michezo inayoendeshwa kisayansi na teknolojia.

### 3.3 Walengwa wa Utafiti

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006: 76) walengwa wa utafiti ni kikundi cha watu au vitu wenye sifa zenye mlingano, japo mdogo, ambao hutumika kama kigezo cha utafiti. Kwa hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu walengwa wa utafiti ni jamii yote ya wakaazi wa Mkunazini na Darajani ambao watakuwa na sifa bainifu zinazohitajika katika utafiti huu. Eneo la Mkunazini na Darajani ni sehemu yenye wakaazi wasiopungua 20,000 lakini utafiti huu ulihusisha watu 60 tu ambao ni wakaazi wa maeneo hayo. Katika jamii hiyo, utafiti umehusisha watoto, wazee na vijana ambao wanapatikana sehemu za mijini ambako ndiko kunakoonekana zaidi kuwa na maendeleo hayo ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Mtafiti amewachagua walengwa hao kwa sababu ya kupata data za aina tofauti kutoka katika makundi na rika tofauti.

#### 3.3.1 Sampuli

Sampuli ni seti ya watu au vitu inayopatikana katika jamii ya watafitiwa ambayo huwa kama kigezo cha jamii ya watafitiwa, (Kombo na Tromp, 2006: 77). Katika utafiti huu, sampuli ni jamii kutoka walengwa wa utafiti ambao wamepata fursa ya

kuwemo kama kigezo katika kukusanya data. Utafiti umetumia idadi ya watu 60 kama ni sampuli wenye mgawanyo unaooneshwa na jadweli ifuatayo:

| **Numb.** | **Sampuli ya Watafitiwa** | **W'ke/ W'me** | **Idadi** |
|---|---|---|---|
| 1. | Wanafunzi wa msingi | 10/ 10 | 20 |
| 2. | Vijana wa mtaani | 10/ 10 | 20 |
| 3. | Wazee (walezi) | 05/ 05 | 10 |
| 4. | Walimu | 05/ 05 | 10 |
| **Jumla** | | **30/ 30** | **60** |

**Jedwali 3. 1**: **Sampuli ya Watafitiwa**

Sampuli ya watafitiwa ilipatikana kwa kutumia mbinu ya sampuli isiyo wakilishi. Hii ni sampuli ambayo inahusisha kila mwana jamii ya watafiti anayo fursa sawa na wenzake katika ushiriki wake. Kwa hivyo, mtafiti aliorodhesha majina yote ya walimu na wanafunzi kwa kuwaweka wanaume mbali na wanawake mbali na baadaye akateua majina yaliyo juu na kuwafanyia utafiti kwa ajili ya kupata data. Kwa upande wa kundi la vijana na wazee, mtafiti alitumia mbinu ya sampuli shirikishi. Hii ni mbinu ambayo mtafiti huteuwa watu maalumu kwa mujibu wa vigezo husika. Mtafiti ametumia mbinu hii kwa sababu sio kila kijana na mzee wa maeneo haya anao ufahamu wa kutosha wa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Kwa hivyo, mtafiti ilimlazimu achague baadhi ya watu ili kuweza kuzipata data zenye kuaminika. Data zilizopatikana kila kundi ziliongeza upeo wa kuelewa athari za maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa nyimbo za watoto waishio mjini katika dhima, uhifadhi na uwasilishaji wake.

### 3.4 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Sehemu hii inaeleza mbinu mbalimbali ambazo zimetumika kukusanyia data pamoja na utaratibu wa mchakato wa kukusanya data.

### 3.4.1 Mbinu ya Usaili

Usaili ni mbinu ambayo mtafiti huwakusanya watafitiwa kwa ajili ya kuwasaili ili kupata data.

Mtafiti ametumia mbinu ya usaili. Katika mbinu hii, mtafiti amewagawa wasailiwa katika makundi manne ambayo ni makundi ya vijana, wazee, walimu na wanafunzi. Mtafiti ametumia maswali tofauti yenye kulingana na kundi husika ili kupata data kwa ufasaha na zenye usahihi. Mtafiti pia ametumia mbinu hii kwa kuwahoji wafanyakazi mbalimbali wa vyombo vya habari wanaoendesha vipindi tofauti vya watoto. Mbinu hii imemsaidia sana mtafiti kupata data zenye kuendana na mada aliyoichagua.

### 3.4.2 Ushuhudiaji

Ushuhudiaji ni mbinu ambayo mtafiti hufika eneo la utafiti na kuangalia matendo yanayofanywa na watafitiwa. Katika mbinu hii mtafiti amebahatika kuhudhuria katika michezo mbalimbali ya watoto na kuona jinsi wanavyoimba na kucheza nyimbo zao hizo. Pia, mtafiti amebahatika kuhudhuria vipindi vinavyofanywa na redio na televisheni Zanzibar na kuona watoto tofauti katika uimbaji na uchezaji wa nyimbo mbalimbali. Mbinu hii imemsaidia sana mtafiti kupata tofauti ya nyimbo zilizokuwa zinaimbwa kabla na baada ya maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano mjini Zanzibar.

### 3.4.3 Udurusu wa Maktaba

Mapitio ya maandishi ni mbinu ambayo inakusanya maandiko kama vile vitabu na ripoti, ambayo yanamilikiwa na mtu binafsi, asasi au shirika (Raj, 2005:153) Maandiko hutupatia taarifa kuhusu mada inayotafitiwa. Mtafiti amepitia maandiko mbalimbali yanayohusu nyimbo za watoto, Sayansi na teknolojia na maendeleo

yake. Kupitia maandiko hayo mtafiti amebahatika kujua historia ya nyimbo za watoto pamoja na utamaduni wa watu wa Zanzibar. Maandiko haya yamemsaidia mtafiti kupata data zenye usahihi ambazo tayari zimeshafanyiwa kazi na wataalamu tofauti duniani.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Katika ukusanyaji wa data, mtafiti ametumia dodoso ndogo na hojaji katika mbinu ya ushuhudiaji na usaili. Katika kuzikusanya data hizo mtafiti ametumia zana mbalimbali kama vile kalamu na karatasi, kinasa sauti, kompyuta na simu ya kiganjani.

#### 3.5.1 Zana za Kukusanyia Data

Utafiti huu umetumia zana zifuatazo;

##### 3.5.1.1 Daftari la Kumbukumbu na Kalamu

Zana hii imetumika wakati wa kukusanyia data mbalimbali zilizohusiana na utafiti huu; mtafiti ameweza kutumia kalamu na daftari ili kupata taarifa zaidi kuhusiana na utafiti huu katika kuandaa madodoso mbalimbali kwa watoto wenyewe, walimu, wazazi pamoja na vijana waishio mijini.

##### 3.5.1.2 Kinasa Sauti

Vile vile, mtafiti ametumia kinasa sauti maneno na nyimbo mbalimbali walizokuwa wakiziimba watoto pamoja na mahojiano kati ya mtafiti na watafitiwa. Zana hii imemsaidia mtafiti katika kuweka kumbukumbu ya maelezo kutoka kwa watafitiwa wakati wa mahojiano na ushuhudiaji wa makini.

#### 3.5.1.3 Simu ya Kiganjani

Pia, mtafiti ametumia simu ya kiganjani kwa ajili ya mawasiliano mbalimbali na watafitiwa pamoja na kupata picha za watoto wawapo michezo mwao wakati wa ushuhudiaji wa makini mtafiti ambapo alikuwepo wakati watoto wakiimba na kucheza michezo yao.

#### 3.5.1.4 Kompyuta

Vile vile, mtafiti ametumia kompyuta kama ni zana moja wapo ya kuhifadhia data ambazo amezikusanya kupitia taarifa mbalimbali za watafitiwa alipokwenda kuwahoji.

## 3.6 Ufaafu na Udhibiti wa Data

Mtafiti amepata ridhaa kwa utawala unaohusika na watu waliohusika na utafiti huu ili watafitiwe. Data zote za uwandani zimekusanywa kwa njia ya mahojiano na udodosaji. Kwa upande wa skuli, madodoso yaligaiwa kwa walimu, watoto kuhusu kuwepo kwa athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia katika nyimbo za watoto.

## 3.7 Masuala ya Maadili ya Utafiti

Mtafiti alizingatia na kufuata mila na utamaduni wa jamii ya watafitiwa. Kwani aliwahoji watafitiwa na kuchukua kumbukumbu kwa ridhaa zao pasi na kuwalazimisha. Aidha, data zote zilizokusanywa katika utafiti huu zitabakia siri kati ya mtafiti na mtafitiwa**.**

## 3.8 Uchambuzi na Uunganishwaji wa Data

Uchambuzi wa data za utafiti huu ulizingatia nadharia ya Usosholojia. Data zimechambuliwa na kupangwa kulingana na malengo ya utafiti wetu. Kila lengo

litakuwa na sehemu yake katika kipengele cha mjadala wa utafiti. Mbinu ya ufafanuzi imetumiwa katika kuchambua data kwa sababu utafiti huo sio wa kitakwimu.

### 3.9 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umeangalia nyimbo za watoto wanazoziimba katika michezo yao. Nyimbo hizo zimehusisha zile za kiasili na zile ambazo zimejitokeza baada ya athari ya sayansi na teknolojia. Utafiti umehusisha maeneo ya mji Mkongwe ukihusisha shehia ya Mkunazini na Darajani.

Utafiti huu ulifanywa kwa sampuli za watoto wenye umri uliotofautiana kuanzia miaka sita hadi kumi na sita. Pia, utafiti huu ulifanywa kwa skuli mbili za binafsi na tatu za Serikali.

Kutokana na uchache wa muda wa utafiti ambao si zaidi ya miezi sita, pamoja na uhaba wa fedha za kujikimu kwa ajili ya kuzunguka maeneo mbalimbali ya mjini, kwa hivyo, ilimlazimu mtafiti kuchagua maeneo hayo pamoja na aina hizo za watafitiwa.

### 3.10 Hitimisho

Sura hii ya utafiti imejadili vipengele mbalimbali ambavyo ni mpango wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli, ukusanyaji wa data, mchakato wa ukusanyaji wa data, uchambuzi na uunganishaji wa data, mipaka ya utafiti na upeo wa utafiti. Kwa hivyo, katika sura itakayofuata itazungumzia uchanganuzi wa data na kutafsiri data zilizokusanywa kwa kina.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI WA DATA NA MJADALA WA MATOKEO.

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii, uwasilishaji, uchambuzi wa data na mjadala wa matokeo umefanyika. Sura hii ya uwasilishaji, uchambuzi wa data na mjadala wa matokeo imechambua na kujadili vipengele vya nyimbo za watoto wa mjini Zanzibar kabla ya sayansi na teknolojia, nyimbo za watoto wa mjini Zanzibar wakati huu, athari za sayansi na teknolojia katika uwasilishaji, athari za sayansi na teknolojia katika dhima na uhifadhi, mchango wa sayansi na teknolojia na kuhitimishia kwa hitimisho.

## 4.1 Uwasilishaji, Uchambuzi wa Data na Mjadala wa Matokeo

Utafiti huu ulifanyika Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar katika maeneo ya Mji Mkongwe ambayo ni Mkunazini na Darajani Unguja na ulikuwa na lengo kuu moja ambalo ni kuchunguza na kubainisha athari za teknolojia ya habari na mawasiliano kwa nyimbo za watoto waishio mjini Zanzibar. Ili kufikia lengo hilo kulikuwa na malengo mahsusi mawili ambayo ni:

i. Kubainisha athari za maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa nyimbo za watoto katika uwasilishaji na dhima.
ii. Kubainisha mchango wa maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika maendeleo ya fasihi simulizi katika utanzu wa watoto mjini Zanzibar.

Ili kupata data zitakazowezesha kutimiza malengo hayo, kulikuwa na maswali mawili ya utafiti huu ambayo ni:

i. Kwa namna gani dhima ya nyimbo za watoto pamoja na uwasilishaji wake vimeathiriwa na maendeleo ya TEHAMA?
ii. Pamoja na athari hizo, nini mchango wa maendeleo ya TEHAMA katika maendeleo ya nyimbo za watoto wa mjini Zanzibar?

Mbinu na zana mbalimbali zilitumika kukusanya data kutoka kwa watafitiwa. Mbinu hizo ni pamoja na mbinu ya mahojiano, ushuhudiaji na kupitia matini mbalimbali. Katika utekelezaji wa mbinu hizo, madodoso mafupi, vinasa sauti, Kompyuta, daftari na kalamu zilitumika kama zana za kukusanyia na kuhifadhia data.

Data zilizokusanywa na kuchambuliwa ni nyimbo za watoto zipatazo kumi na nne zikiwemo saba za Bongo Fleva ambazo watoto wa mjini huziimba katika michezo yao pamoja na taarifa zinazohusu nyimbo hizo na maoni ya watafitiwa mbalimbali waliozungumza na mtafiti. Uwasilishaji, Uchambuzi wa data pamoja na mjadala wa matokeo umefanywa kulingana na malengo ya utafiti huu.

Katika mchakato wa mjadala wa uchambuzi wa data, mtafiti alihojiana na watafitiwa na kupata data mbalimbali. Katika mjadala huo wazazi nao waliongea kuwa, ingawa sayansi na teknolojia ina faida kwa mwanadamu, kwa vile ni chombo cha kurahisisha utendaji wa kazi, lakini kwa kiasi kikubwa sana yameathiri fasihi simulizi ambapo nyimbo za watoto ni miongoni mwa aina ya fasihi simulizi iliyoathiriwa na maendeleo hayo. Wamesema, watoto wengi ambao wamezaliwa na kukulia maeneo ya mijini, ndio waathirika wakubwa wa maendeleo hayo kwa sababu wamekosa ile fursa adhimu ya kuimbiwa na kusimuliwa hadithi na bibi, babu, mama na dada zao nyakati za usiku. Badala yake ni kusikiliza radio, kuangalia runinga na kufungua intaneti.

Hata hivyo, maendeleo hayo yamesaidia kutopotea kwa fasihi simulizi ya kitoto kwani imetoa mchango mkubwa wa uhifadhi wa nyimbo hizo ingawa kwa njia hiyo ya uhifadhi inapoteza uasili wake, kwani kabla ya kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, nyimbo zote za watoto zilikuwa zikihifadhiwa kichwani tu. Siku hizi uhifadhi na uendelezaji wa nyimbo za watoto umekuwa wa kudumu. Leo hii wimbo wowote unaweza kuhifadhiwa kwenye mkanda, santuri, video, televisheni au kompyuta na ukarushwa hewani na kuwapata wasikilizaji na watazamaji wengi. Uhifadhi huu unasaidia wimbo kudumu kwa miaka mingi hata kama aliyeimba wimbo huo amefariki. Hivyo basi, swala la nyimbo za watoto kupotea baada ya mwimbaji/fanani kufa huepukika kutokana na hadhira kuweza kusikia sauti au kuangalia matendo ya fanani yaliyohifadhiwa katika mkanda wa santuri, video au runinga.

### 4.1.2 Nyimbo za Watoto wa Zanzibar Mjini

Nyimbo za watoto zimejadiliwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi. Kuna aina mbalimbali za nyimbo zinazopatikana katika jamii nyingi duniani kote. Aina hizo za nyimbo hujitokeza kutokana na dhima pamoja na uumbaji wake. Kwa mfano nyimbo za chekechea, nyimbo za michezo na nyimbo bembelezi. Zote hizi ni miongoni mwa nyimbo za watoto lakini hujitofautisha kidhima na kiuwasilishaji kulingana na mazingira, wakati na maudhui kwa mujibu wa jamii husika. Mtafiti amebahatika kukaa kwa makini na kuangalia watoto wakiimba na kucheza michezo mbalimbali kwa mfano, ***Foliti.***

Mwimbaji: Foliti × 2
Waitikiaji: Badia × 2
Mwimbaji: Nikija ntampata nani?
Waitikiaji: Asha na kidudu mtu
Mwimbaji: Nije nsije?
Waitikiaji: Njoo
Mwimbaji: Kwa miguu mingapi?
Waitikiaji: Mitatu

***Chanzo: wanafunzi wa skuli 23/02/2015***

Mchezo huu ni wa kale unaoambatana na wimbo unaoitwa foliti. Aghalabu, mchezo huu huchezwa wakati wa mchana au usiku wa mapema wa mbalamwezi. Wimbo huu huimbwa ikiwa watoto wametawanyika katika eneo moja na baadaye mmoja huwa anawafukuza wenzake baada ya kumalizia wimbo kwa kusema, “nije kwa miguu mingapi?” Waitikiaji wanapotoa kauli ya “njoo kwa miguu mitatu”, hapo mwimbaji huanza kuwafukuza hadi atakapompata wa kumkamata wanabadilishana zamu. Yule aliyekamatwa anakuwa sasa ndie mwimbaji na kufukuza wenzake hadi watakapochoka na kuamua kupumzika.

Mtafiti baada ya kuangalia kwa kina mchezo na wimbo wake, alipata fursa ya kuwahoji baadhi ya watoto sababu zilizowafanya wacheze na kuimba mchezo huu, kwani kwa mtafiti aliona kama kwamba watoto wanajitesa baada ya kuamua kufukuzana kwani baadhi yao wanakuwa wanaanguka baada ya kupigana kumbo na wenzao. Watoto hao walikuwa na haya ya kusema;

> “Mwalimu wetu katwambia tukacheze hivyo tunapata furaha na kuchangamsha mwili baada ya kusoma”

Mtafiti alibahatika kukutana na watoto na kuwahoji waimbe wimbo wowote wanaoujua ambao wameshawahi kuuona au kuusikia ukiimbwa katika vyombo vya habari. Mtoto mmoja alimuimbia mtafiti wimbo wa ***Kinyulinyuli*** ulioimbwa na msanii wa Bongo fleva anaejulikana kwa jina la Samir. Wimbo huu unaosema:

Ni bora uwe mchoyo
Nisikufume kwenye kichochoro
Usiniweke kiporo
Ukajazua mgogoro
Nikupeleke nyashiro
Tukale wote ng’arambo
Kama klabu twende Sansiro
Ninakupa sana mabaro
Kule utamu kunoga
Wenye ladha kama bagaa
Wanasema umeniroga

Umenifanya ndondochaaa
Mami wewe ni maji
Kwenye jangwaaa
Ifungue dibaji unisomeee
Usinidengulieee
Kinyuli nyuulii nyulika × 2
Kidali kikidaliii kidalipo × 2
Njoo tucheze kinyuli nyuuliii nyulika
Kinyuli nyuuliii nyulika……………………

***Chanzo: wanafunzi wa skuli 23/02/2015***

Wimbo huu asili yake ni wimbo wa watoto Kinyulinyulika, lakini kutokana na maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano unaimbwa na mtu mzima na unatumia ala mbalimbali za muziki, hali ambayo kwa watafitiwa waliohojiwa waliobahatika wameeleza kuwa wimbo umepoteza asili ya wimbo wa watoto na kilichobakia ni kutumia tu maneno ya nyimbo za watoto.Kama inavyobainishwa na wimbo huu.

Kinyuliii nyulika
Mwanangu mwanajumbe
Kava nguo mbili
Ya tatu kajibandika
Ukakasii na urembo
Aliye juu na usheee

***Chanzo: wazazi 09/11/2014***

Wimbo huu huimbwa na kikundi cha watoto ambao hukaa kitako chini na kupachika mikono yao mmoja juu ya mwengine, kwa kutumia ncha za vidole kwa mfano wa kunyukuana. Huimba wimbo huo kwa kumtaka aliyeweka mkono wake juu auondoshe mpaka anabakia wa mwisho kabisa. Yule anayebaki mwisho huchukuliwa mkono wake na kusagwa sagwa chini huku akiimbiwa "kasaga mavi kwa mkono". Hapo mchezo humalizika kwa furaha kabisa bila ya ugomvi. Mfano, picha 4.1 ni kielelezo cha picha ya watoto wakiimba wimbo wa ***Kinyulinyulika.***



**Picha 1: Watoto wa mtaa wa Mkunazini wanaonekana wakicheza na kuimba wimbo wa Kinyulinyulika, (chanzo mtafiti 14/2/2015)**

Hivyo, kwa kuwa kila mwanadamu katika vipindi mbalimbali vya maisha huwa na mahitaji maalum katika maisha, watoto nao huhitaji mambo mbali mbali ikiwemo michezo. Mara nyingi michezo waichezayo watoto huambatana na nyimbo ambazo huwaburudisha na kuwaelimisha. Nyimbo hizo waziimbazo katika michezo yao huwasaidia katika kuimarisha na kuwakuza kiakili.Ujuzi mwingi walionao watoto katika utambuzi wa kujua mambo unatokana na baadhi ya nyimbo ambazo watoto wanaziimba katika michezo yao. Nyimbo hizo huwafanya watoto wawe na udadisi zaidi. Kwa mfano, baadhi ya nyimbo waziimbazo watoto hujifunza kurithishana wao wenyewe toka kizazi kimoja hadi kingine.

Uhifadhi na uthabiti wa nyimbo za watoto waishio mijini katika muktadha wa maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano umeweza kusaidia katika kuhifadhi vizuri nyimbo za watoto kuliko ilivyofikiriwa na wanamapokeo.Uthabiti wake ni wa kudumu, kwani leo hii nyimbo nyingi zinawekwa kwenye vifaa mbalimbali kama vile kompyuta, (flopy/flash), mikanda ya santuri na video au

katika CD. Hivyo nyimbo zinakuwa zinaendelea kuwepo kwa muda mrefu sana sawa na fasihi andishi inavyokuwa inahifadhiwa katika maandishi. Kwa upande wa video uhifadhi wake huendelea kuonesha vitendo na sauti na huweza kudumu hata zaidi ya maandishi kama zitatumiwa vizuri.

Ufafanuzi wa Utandawazi umekuwa ukitegemea zaidi mtazamo wa mtu ambaye anaifasili dhana yenyewe.Wataalamu mbali mbali wameifasili dhana hii kutokana na mitazamo mbali mbali. Ama kama ilivyodhihirishwa na maoni ya wataalamu, dhana ya utandawazi ni pana sana na imekuwepo katika nyanja mbalimbali katika maisha ya mwanadamu. Maendeleo ya sayansi na teknolojia hasa katika teknolojia ya habari na mawasiliano yameigeuza dunia kuwa ndogo mithili ya kijiji katika mawasiliano kwani matukio yanayofanyika ulimwenguni kote huweza kusikika au kuonekana kwa muda ule ule tukio linapotokea kwa watu wa ulimwengu mzima kutokana teknolojia hii ya mawasiliano.

Halikadhalika, kwa mujibu wa Chachage (2004), utandawazi ni dhana ambayo imewateka wasomi, wanasiasa, wanauchumi na waandishi wa habari barani Afrika wakiwemo na watoto.

Utandawazi ni mkakakati wa makusudi uliopangwa na wenye nguvu ambao unalazimisha serikali na watu kutawaliwa na wenye nguvu za kiuchumi na kijamii ambazo zinadaiwa kwamba hazizimiki wala kupingika (Chachage 2004:43)

Utandawazi ni jambo linalolenga umiliki wa kifikra na kiutamaduni juu ya tamaduni nyingine zilizodhaifu, kwa ajili ya kusaidiana, kuungana yaani kuwa kitu kimoja, kuondoa mipaka na masafa baina ya nchi na nchi, kukusanyika pamoja na kuleta kitu kinachoitwa “kijiji ulimwengu”. Dhana hii ndiyo iliyoathiri nyimbo za watoto

waishio mijini ambako maendeleo haya ya teknolojia ya habari na mawasiliano imeenea zaidi.

Katika ufafanuzi wa dhana hii utandawazi, neno muhimu ni “uunganishwaji”. Hii ina maana kuwa watu wa sehemu moja wanakuwa wanahusiana na watu wa sehemu nyengine. Jambo lililodhahiri ni kwamba dhana ya utandawazi chimbuko lake ni katika nchi za magharibi ambazo zimeendelea zaidi katika mfumo mzima wa mawasiliano. Nchi nyingi za magharibi yaani Marekani na Ulaya, ni nchi zenye maendeleo zaidi katika mfumo wa mawasiliano ambao ndio umeenea duniani kote na kusababisha athari nyingi katika nyimbo za watoto waishio mijini.

Katika tasnifu hii, mtafiti ameafikiana na wataalamu mbalimbali waliotoa fasili ya utandawazi kutokana na dhana yenyewe kuwa pana. Hivyo, mtafiti ameona kuwa yenye kushabihiana na utafiti huu ni lazima katika teknolojia ya habari na mawasiliano ambayo inahusisha usambazaji wa habari ambayo ndiyo umeathiri nyimbo za watoto waishio maeneo mijini.

#### 4.1.2.1 Historia ya Nyimbo za Watoto Kabla na Baada ya Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia

Kwa mujibu wa wazee mbalimbali waliohojiwa wamesema kuwa, nyimbo za watoto ni maarufu sana katika jamii ya Kizanzibari na ni nadra sana kuwakuta watoto wanacheza wasiingize nyimbo katika michezo yao.

Nyimbo za watoto aghalabu, huambatana na kucheza, ambapo kunaleta ladha fulani kwa atakaeekaa kuangalia jinsi watoto hao wanapocheza. Ili kuelewa athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa nyimbo za watoto wa mjini Zanzibar ni jambo la muhimu kuziangalia nyimbo hizo katika muktadha wa kihistoria.

Pia wameeleza kuwa nyimbo za watoto husheheni mawazo mazito na hudhamiria kuonesha uhusiano wa kijamii, migogoro ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kwa kupitia nyimbo hizo, watoto hubadilika, huburudika, hujifunza, huomboleza na hupitisha amali za jamii na historia.

Baada ya mahojiano, mtafiti alielezwa kuwa, historia ya nyimbo za watoto Zanzibar ilianza kwa masimulizi ya moja kwa moja (ana kwa ana). Mmojawao alisema kuwa, mwanzilishi wa nyimbo hizi za watoto ni Siti binti Saadi, ambaye alitunga nyimbo hizo kwa lengo la kuwafurahisha na kuwaburudisha watoto, baadaye nyimbo hizo zilirithiwa na watoto na hapo watu wakaona kuwa nyimbo hizo zimetokana na watoto wenyewe na kwa vile fasihi simulizi haina mrithi maalumu, ni mali ya jamii, hivyo, zikaonekana kuwa ni zao la watoto. Ingawa huo ndio uhalisia, lakini kitu chochote lazima kiwe na chanzo chake, kwa hivyo, walisisitiza kuwa, nyimbo za watoto nazo chanzo chake ni Siti binti Saadi. Mwendelezo wa nyimbo hizo ulikuwa ni wa watoto wenyewe baada ya kuwekewa misingi imara na madhubuti na gwiji huyo wa sanaa. Nyimbo hizo za watoto zilikuwa zinawasilishwa kwa mdomo ambapo fanani na hadhira walikuwa wanapokezana na wakati mwengine kushirikiana katika uimbaji wao. Hali hiyo ilikuwa ikijenga ucheshi, uchangamfu na ujasiri katika uwasilishwaji wake, matokeo mengi katika uwasilishaji wa nyimbo hizo hujitokeza wakati wa kufukuzana, kujificha na kuvutana.

Nyimbo za watoto zilitumika kuwajenga watoto kimaadili na kiafya ili wawe jasiri, wastahamilivu, wazalendo, kuwa na umoja, ushirikiano na kupendana. Kwa hivyo, nyimbo nyingi walizokuwa wanaimba watoto wenyewe au kuimbiwa na wazazi wao zilikuwa zinahimiza mambo hayo. Kwa mfano wimbo wa ***Howani***

Howani mama howaniiii
Kitunguu na ubaniiiii

Nyoka kalala njianiiii
Tumkanyage kichwaniiii
Apishe wendao majiiii
Na wendao kata kuniii

***Chanzo: Mzazi, 20/02/2015***

Wimbo huu wazazi walikuwa wanawaimbia watoto wao kuwajengea ujasiri na ustahamilivu. Mara nyingi mama au mlezi huimba wimbo huu wakati mtoto wake analia, humbembeleza kwa kumtaka anyamaze au alale, (licha ya kuwa mtoto huyo hafahamu aimbiwacho na mama yake), mama humtaka mtoto huyo aweze kupambana na hali ya maisha kuwa anaweza kukabiliana na vikwazo, na utatuzi wa vikwazo hivyo ni ustahamilivu kwa mfano pale anaposema;

Nyoka kalala njiani
Tumkanyage kichwani

Mama hakumwambia mtoto wake akimbie ila alimtaka kumkanyaga nyoka aendelee na safari yake, hii ina maana ya kwamba katika maisha hakuna mema matupu atakumbana na vikwazo mbalimbali ambavyo anatakiwa kupambana navyo kwa njia moja au nyingine na sio kukimbia shida zinapomfikia. Pia baadhi ya nyimbo hizo za watoto hutoa maonyo kwa watoto wakati wanapotaka kufanya mambo yaliyowazidi kimo, kwa mfano wimbo wa ***Mzigo Mzito;***

Nilikwambia zamaniii
Kama mzigo mzitoooo
Ukanambia nitwikeeee
Japo robo ya kipetoooo
Songa kata nikutwikeee
Jaala ni jambo zitooo

***Chanzo: Watoto mtaani, 15/04/2015***

Vile vile baadhi ya nyimbo hizo za watoto huhimiza upendo kwa mama na mtoto wake, hilo haliishii kwa mama na mtoto bali huwahimiza watoto wapendane. Mfano wa nyimbo hizo ni;

Pepo tua × 2
Mwanangu yu baharinii
Arudipo × 2
Salama usalimini
Nna nadhiri naweka ya kombe msikitini
***Chanzo: Mzazi, 20/02/2015***

Mama hapa anajaribu kumuombea salama mwanawe ambaye ameenda kutafuta maisha kwamba endapo atafanikiwa basi atamuombea dua azidi kupata mafanikio.

Baadaye msanii Siti binti Sadi alianza kutunga nyimbo za watu wazima na kuwaburudisha kama vile ***Muhogo wa Jang'ombe, Kijiti*** na nyinginezo ambazo zimekuja kurithiwa na msanii mkongwe na maarufu almarhumu Fatma binti Baraka maarufu Bikidude.

Baada ya kupata maendeleo katika visiwa vya Zanzibar, teknolojia ya habari na mawasiliano kama vile radio na televisheni, utanzu huu nao ulianza kufuata mkumbo na kuanza kuimbwa kupitia vyombo vya habari na kuandikwa kupitia vitabu, magazeti na majarida mbalimbali. Hali hiyo si tu ilihifadhi na kutumia nyimbo za watoto, bali pia kwa upande wa pili, zilianza kupungua kasi na uasili wa utanzu huu.

Kuanzia hapo watoto walianza kupungua kuzitumia nyimbo hizo, na kwa wakati huu ni nadra sana kumsikia mama anambembeleza mtoto wake kwa nyimbo za watoto za zamani badala yake huimba nyimbo mbalimbali za kisasa kama vile taarabu, bongo fleva na kadhalika.

Mnamo miaka ya 2000, utanzu huu ndio umeonekana kupotea kwa kiasi kikubwa sana kwani redio Zanzibar ilianzisha kipindi cha TUSOME TUJIFUNZE ambapo

walizitumia nyimbo mbalimbali za watoto katika kufundishia na kujifunza. Nyimbo hizo zilikuwa zinaimbwa radioni zikiwa na ala za muziki.

Hali hiyo imesababisha watoto kuanza kuziimba nyimbo hizo kwa kuziiga radioni pasi na kujua dhima na uwasilishaji wake. Hata hivyo, imeelezwa na watafitiwa kuwa wazazi wengi wa watoto wa mitaani wanashindwa kuziimba nyimbo hizo za watoto kama zilivyokuwa, pamoja na kuzicheza badala yake wamejikuta wakivamia nyimbo mbalimbali zinazoimbwa katika vyombo vya habari. Kwa hivyo, kwa miaka hii sio ajabu kumkuta mtoto wa miaka mitano (5), hadi kumi na saba (17), kuimba wimbo wa kimapenzi unaoimbwa kupitia radio na televisheni

#### 4.1.2.2 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Uwasilishaji.

Watafitiwa wameeleza kuwa matini ya nyimbo nyingi waziimbazo watoto waishio mijini zimeathiriwa na kuwepo kwa maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Athari za muziki wa kizazi kipya, zinatokana na kuenea kwa maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA). Katika kuimba na kutunga nyimbo zao, watoto waishio mijini huwa wanaiga nyimbo zinazoimbwa na kusikika katika vyombo vya habari na mawasiliano kama radio na televisheni. Watoto huiga muundo, uimbaji, uchezaji na hata kujipa majina ya kisanii kama wafanyavyo wasanii mbalimbali wa muziki wa kizazi kipya hapa nchini Tanzania.

Mfano mzuri ni msanii chipukizi wa Kibongo ambae anaonekana kuvuma sana na kujipatia umaarufu ingawa bado ni mtoto wa miaka kumi na sita tu. Hayo, yameelezwa na mtafitiwa kwa kusema kuwa, Dogo Aslay ni mtoto ambaye amejaaliwa kuwa na kipaji tangu utotoni mwake, ni mwanafunzi maskini ambaye mbali ya kuwa na wazazi wake, familia yake inamtegemea kwa hali na mali, hivyo basi, akaona ipo haja ya kutumia kipaji chake hicho ili kujikwamua kimaisha yeye

na wazazi wazazi wake. Ameanza kuimba akiwa na umri wa miaka kumi na nne (14) hadi sasa ana umri wa miaka kumi na sita (16). Mwanzoni alianza kuimba nyimbo za kitoto ambapo alikuwa akiimba peke yake na wimbo wake wa mwanzo unajulikana kwa jina la “Naenda Kusema kwa Mama”. Kwa sasa kijana huyo ameacha shule na anaendeleza fani yake ya uimbaji akiwa katika kundi zima linalojulikana kwa jina la “YA MOTO BAND”.

Mfano wa wimbo ***Naenda Kusema kwa Mama:***

Tena inaniumaaaa kwa sana leeo
Nikitoka naenda kumwambia mama leeo
Naenda kuseeema kwa mama kuseemaaa

Nyumbani mama umemwachia buku
Kishtobe ba umemnunulia kuku
Ukirudi nyumbani mikono mitupu
Tena kurudi kwako ni usiku
Inaniuma naseeema
Sinyamazi hata uninunulie nyama
Akununulie nani nyama
Utakula hilo hilo dagaa

Leo nyumbaani patachimbiiika
Nitamwambia hadi sehemu uliyotoka
Nasema leo mbona patanuka
Namweleza mama pamoja na kaka
Wewe mbona sie unatutesa
Unaondoka hutuachii hata pesaaaa
Namweleza yote yako makosa
Pengine utakuja kuyaachaaa
Watoto mliozaliwa wakati huu
wa Jakaya yuko madarakani mnashidaa
Naseema nasema inaniuma sanaaaaa
Kila siku nyumbani kugombana

***Chanzo: Mtayarishaji kipindi cha vijana na muziki Z.B.C.T.V. tarehe 12/2/2015***

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyoenea Tanzania, hususan maeneo ya mijini, ndiyo yaliyosababisha kuathiri nyimbo za watoto wengi wanaoishi mijini, kutokana

na matumizi ya vyombo vya habari kama vile televisheni, redio, magazeti na majarida mbalimbali kutoa nyimbo tofauti ambazo ndizo zinaigwa na kuimbwa na watoto. Mtoto Aslay alibainisha kuwa ameathiriwa na waimbaji wa muziki wa kizazi kipya ndipo akaona ipo haja na yeye kujiingiza katika ulimwengu wa muziki kutokana na kipaji alichonacho.

Uteuzi wa maneno katika nyimbo za watoto ni ufundi wanaoutumia katika kuchagua maneno yanayotumiwa katika nyimbo zao. Ufundi huu umeonesha kuwa, kwa kiasi kikubwa, katika nyimbo nyingi wanazozitunga na kuziimba, umeathiriwa na uteuzi wa maneno wayatumiayo wasanii mbalimbali hapa nchini Tanzania, ambao nyimbo zao husikika sana kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mawasiliano vinavyopatikana maeneo ya mijini. Maneno haya yameelezwa na baadhi ya wazazi wa watoto wanaoishi maeneo ya Mkunazini mjini Unguja, walipohojiwa. Vile vile, wamesema, nyimbo nyingi za watoto zimebainika kuwa na matumizi ya lugha nyepesi ambayo inatumika hata katika matumizi ya watu. Baadhi ya nyimbo ambazo mtafiti amezichunguza, amebaini kuwa watoto wamezitunga kwa kutumia lugha wanayoitumia katika mazungumzo yao ya kawaida, ijapokuwa zinakuwa na mahadhi ya kuiga au kufananisha na nyimbo waziimbazo wasanii mbalimbali na kurushwa hewani na vyombo vya habari na mawasiliano. Maneno wanayoyatumia watoto katika utunzi na uimbaji wa baadhi ya nyimbo zao, unafuata mitindo mbalimbali wa nyimbo ambazo zinaimbwa na wasanii wa muziki wa kizazi kipya hapa nchini Tanzania. Mahadhi ya baadhi ya nyimbo kama vile mpangilio wa sauti na maneno unafanana na mpangilio wa sauti na maneno wa nyimbo wanazozisikia kupitia vyombo vya habari na mawasiliano vilivyopo katika maeneo wanayoishi.

Katika michezo yao watoto walikuwa wakiimba wimbo uliofananishwa na wimbo wa kizazi kipya kimuundo kwani wasanii wa kizazi kipya mara nyingi wanapotunga nyimbo zao hulazimisha ziwe na vina vinavofanana hata kama havina mantiki, kulithibitisha hili tuangalie mfano ufuatao:

Mama wa kambo mbo
Mbona wanitesa sa
Sasa naondoka ka
Kaa peke yako ko
Koma kunipiga ga
Gari ya baba ba
Baba wa Taifa fa
Fagia uwanja nja
Njaa inauma ma
Mama mzazi zi
Zizi la ng'ombe mbe
Mbele kuna kiza za
Zahabu yang'ara ra
Rangi nyeupe pe…

***Chanzo: mwanafunzi wa skuli ya Mkunazini, 13/2/2015***

Katika wimbo huu umetumika mtindo ambapo kina kinachomalizia ndicho kinachoanzia mstari unaofuata kwa mfano, mstari wa tatu kutoka chini umemalizia na *za* ambapo mstari unaofuata chini umeanzia na *za* kwa kuunda neno "zahabu".

Hivyo, katika utafiti huu, mtafiti ameweza kubaini kuwa uteuzi wa maneno katika nyimbo nyingi wazitungazo na kuziimba watoto waishio mijini ni athari ya kuwepo kwa vyombo vya habari na mawasiliano, ambavyo hurusha hewani nyimbo nyingi za wasanii wa kizazi kipya. Watoto wanatumia maneno mengi yanayotumiwa na wasanii hao wa kizazi kipya (Bongo Fleva), ingawa baadhi yao hutumia ubunifu mkubwa zaidi.

Halikadhalika, katika uteuzi wa maneno hutumia maneno machache. Nyimbo nyingi ambazo mtafiti amezichunguza amezibaini kuwa ni fupi fupi na zenye kutumia

maneno machache. Nyimbo hizo zimeathiriwa na nyimbo fupi za wasanii waliowasikia au kuwaona kupitia televisheni. Mfano wa wimbo wa kizazi kipya ambao uliimbwa na kikundi cha Two Berry ambacho ni muungano wa wasanii wawili ambao wanaitwa Mbarak.

Minataka kuwa nawe kuwa nawewe tu
Ulonifanya kuwa nawe kuwa na wewe tu
Mpenzi wangu nakupenda
Mimi kwa mwengine stokwenda
Kukufata sitochoka popote pale we utapokwenda
Watu wananita zoba
Wanasema eti umeniroga
Watasema watachonga ujue bado mimi nakupenda aaaa

Nitazame nilivyokonda
Yote kwa sababu nakupenda
Kukuwaza sitochoka
Milele mi moyoni takuweka
Watu wanachonga sana
Wanasema umenipa limbwata
Hata kama wanasema ujue bado nakupendaaaaa

***Chanzo: Vijana wa Mtaa, tarehe, 20/01/2015.***

Wimbo hii ingawa unaonekana ni refu lakini una maneno machache yenye kujirudia rudia hivyo kuuona kuwa kubwa sana. Wimbo huu umeuathiri wimbo wa watoto ***Alfola*** kwa kuwafanya watoto badala ya kuimba wimbo wao wa asili ***Alfola*** wanaimba wimbo ulioimbwa na wasanii wa kizazi kipya Zanzibar Berry black na Berry white katika kundi zima la “Two Berry” unaokwenda kwa jina la ***Nataka kuwa na wewe***. Hivyo, watoto huuimba wimbo huo katika michezo yao. Mfano wa wimbo wa watoto;

Alfola Alfola
Alfola bandar salama
Alfola imekufa
Imebakia mifupa
Kiguru cheche
Cheche cheche
Alo na donda

Tumtoneshe
Alo na jipu
Tumtumbue

***Chanzo: Mzazi, 20/02/2015***

Wimbo huu huimbwa na watoto wakiwa wamekamatana mikono hadi wanapofikia kipande kinachosema ***Kiguru cheche*** wanaruka ruka kwa mguu mmoja na kila mtu kurusha mguu wake kwa kuhofia asije kukanyagwa na mwenzake. Kutokana na athari ya wimbo ***Nataka Kuwa na Wewe,*** inaonekana dhahiri kwamba wimbo huu umeshapoteza uasili wake.

Uwasilishaji wa nyimbo za watoto kwa kutumia matumizi ya lugha ya matusi katika karne hii ya sayansi na teknolojia inaonekana kushika kasi kama Mwalimu wa skuli ya msingi Mkunazini aliyobainisha (tarehe, 7/2/2015). Kutokana na watoto kuzisikia na kuziona nyimbo mbalimbali zinazorushwa hewani na vyombo vya habari zikiwa zimesheheni lugha za matusi na aibu, watoto nao wanaiga mwenendo huo kwa kuona kuwa ni lugha ya kawaida kwa sababu wanazisikia zikiimbwa bila ya kificho.

Mfano wa wimbo wa watoto

Kama dada wanipenda kaninunulie zeze
Nikilala kitandani zeze linibembeleze
Mama nalia kusema sema kubaya
Utamsema mkweo alokuzalia mumeo
Kadi kanya kadi kanya kadi
Namuogopa Ali kadi kanya kadi kanya
Atanilaza chali kadi kanya kadi kanya
Katikati ya bahari kadi kanya kadi kanya
Namuogopa Juma kadi kanya kadi kanya
Atanipiga chuma.

***Chanzo: Mwalimu wa Skuli ya Mkunazini tarehe, 7/2/2015),***

Wimbo huu huambatana na mchezo ambao huchezwa na watoto wawili, katika mchezo huo watoto hao hukamatana mikono yao; baadaye wakacheza kwa kupishana, hadi wanapofika pale wanaposema “kadikanya” hunyanyuka na kuanza kuchezesha viungo vyao. Watoto huufurahia smchezo huu kwani wanapata mazoezi ndani yake, lakini pia unatoa mafunzo ya kwamba wasicheze na watoto wanaume kwani huenda ikatokea athari kubwa kwa mfano pale waliposema “ namuogopa Ali atanilaza chali” na “namuogopa Juma atanipiga chuma”.

Wimbo wa ***Selina*** ulioimbwa na msanii wa kizazi kipya Alicom na Selina ni kigezo kikubwa kinachoonesha kuwa wasanii hao hutumia lugha ya matusi tena kwa uwazi kabisa, ambapo vyombo vya habari bila ya kuchuja matusi hayo huzirusha hewani nyimbo za wasanii bila kuangalia athari itakayojitokeza kwa watoto: Mfano wa nyimbo za aina hii ni wimbo ufuatao:

Nikitafakari penzi unalonipa Selina
kukuacha mi siwezi jua kwako jilisina
Hata mi nimetembea
wengi nimejionea macho kinikodolea ila kwako nimekolea
Nishike mkono nikubusu
hata kiuno mali yako
Nataka shavu na ulimi
pia viko kwa ajili yako
Macho yako kama ya gololi
kifua chako kinanizingua
Sura yako Seli ya mdoli
sauti yako inanivutia

Mwili hunisisimka ukinibusu shavuni
mimi hoi taabani
Hata mi wanizingua ukinishika kiuno
mwili ukinichezea nnalala kama pono
Basi njoo unigae joto
nami nitoe kwenye baridi
Nikipi kinakupa mvuto
nimapenzi hakuna zaidi
Kwetu umekwisha kubalika
hata nawe kwetu huna shaka

Basi njoo kwetu Malaika
usihofu nimekwisha fika
Wapambe tusiwakubali
Mimi nawe tushikamane
Tusisikilize uzushi
Nia yao tufarakane
Seli wangu we kimwana
Nataka tufunge ndoa
Unizalie na wana
Nitakapo kuowa

***Chanzo: Mwalim wa Skuli ya Mkunazini, tarehe, 7/2/2015),***

Wimbo huu wa Alicom na mwenzake umetumia lugha ya matusi ya uwazi kabisa ambapo, inapoimbwa wimbo huu mbele ya wazazi unaweza kujichimbia shimo ukaingia kwa aibu utakayoipata. Kwa muda huu wa utandawazi vijana wanaona ni lugha ya kawaida sana kwa sababu ni rahisi kujipatia soko kwa sababu wasikilizaji na watazamaji kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Aidha watoto wataupenda kuusikiliza na kuuona, kwani wimbo huu unawagusa wapendanao jambo ambalo kwa sasa si geni. Hii ni moja ya athari ya utandawazi ambao unaenezwa zaidi na vyombo vya habari. Mwalimu mmoja katika Skuli ya Darajani Unguja akimueleza mtafiti kwamba miongoni mwa athari za sayansi na teknolojia ni kuzungumza mambo kwa uwazi pasi na tone la haya, vijana baada kuyasikia haya wanayashabikia kiasi ambacho husababisha kuporomoka kwa maadili.

Maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo yameenea zaidi maeneo ya mjini, ambayo ndiyo yamesababisha kukua na kuenea kwa utandawazi. Maendeleo hayo yameathiri nyimbo za watoto waishio mijini. Utandawazi umeathiri sana watoto katika jamii, hususan katika nyimbo zao. Katika kuchunguza mtafiti amebaini kuwa nyimbo mbalimbali za wasanii wanatumia lugha isiyo na stara.

Kwa mujibu wa majumuisho ya madodoso, watafitiwa wengi wamemueleza mtafiti kwamba, wasanii huchanganya lugha nyingine katika nyimbo zao ambazo huimbwa kwa lugha ya Kiswahili na kufanya kutumika kama Kiswahili. Utandawazi umeathiri lugha ya Kiswahili kwa kuzalisha viswahili ambavyo ndiyo chanzo cha kuihairibu lugha hiyo na kuporomosha maadili ya Kiswahili.

Watoto huiga matumizi ya Kiswahili kinachokiuka utaratibu katika utunzi na uimbaji wa nyimbo zao. Baadhi ya vyombo vya habari hapa nchini Tanzania, vimekuwa vikitumia lugha ya Kiswahili kwa kuchanganya maneno ya lugha ya Kiswahili na lugha za kigeni, kama vile lugha ya Kiingereza. Watoto waishio mijini hutunga na kuimba nyimbo zao zikiwa na mchanganyiko wa lugha.

Mfano wa nyimbo za watoto

Oni suny sa mazde
How the children play
Oni suny sa mazde
Wakati wa jua kali zde
Hao watoto watizama ndege zde

***Chanzo: Mwalim wa Skuli ya Mkunazini 17/11/2014***

Huu ni wimbo wa watoto ambao wameutunga kwa kuchanganya lugha mbili ya Kiswahili na Kiingereza. Hii ni athari inayotokana na nyimbo za wasanii wa kizazi kipya ambako ndiko watoto mara nyingi wanakoiga. Wasanii hutumia lugha mchanganyiko kwa kutaka kuonesha umahiri wao katika fani zao bila ya kujali athari gani huweza kujitokeza wanapochanganya lugha mbili hizo au zaidi. Miongoni mwa wasanii wanaopenda kuchanganya lugha katika nyimbo zao ni msanii maarufu wa kike Judith Wambura kwa jina la kisanii ni Lady J dee au Jide. Tuangalie mfano ufuatao wa msanii huyo.

I forever rever love you, never leave you go ooh
I forever rever love you, never leave you go ooh
I want you know ooooh
Haya mapenzi ya kweli
Acha skele sbeiye
Utanielewa vipi
Moyo wangu wote uko kwako
Wona mara mi baby ya craby
Nnapotoka tu tusipikwepo tu
Moyo wangu wakufaaaata
I forever rever love me, never leave me go oooh
I forever rever love me, never leave me go oooh

***Chanzo: Mwalim wa Skuli ya Mkunazini 17/11/2014***

Katika wimbo huu mtafiti ameona dhahiri ni jinsi gani msanii huyo amechanganya lugha mbili hizo kutokana na kuathiriwa kwake na sayansi na teknolojia ambayo inaonekana kuota mizizi nchini Tanzania.

Aidha, ucheshi ni mbinu wanazotumia wasanii katika nyimbo. wasanii huchagua maneno ambayo yanawachekesha na kuwaburudisha hadhira ili kuongeza wapenzi na kupata soko. Miongoni mwa mambo ya msingi ambayo hujitokeza katika uwasilishaji wa nyimbo za watoto ni ucheshi. Ucheshi unawajenga watoto kiakili na kiwiliwili. Ucheshi unaweza kujitokeza katika hali ya kufikiri. Mfano;

Gari ya baba ba
Baba wa Taifa fa
Fagia uwanja nja
Njaa inauma ma
Mama mzazi zi
Zizi la ng’ombe mbe
Mbele kuna kiza za
Zahabu yang’ara ra

***Chanzo: watoto wa skuli ya Mkunazini 13/2/2015***

Katika wimbo huu mtoto mbali ya kuchangamka na kufurahi bali pia huweza kutumia akili yake kwa kuzalisha maneno ambayo yanafanana na kina kilichomalizia katika ubeti. Ingawa watoto huburudika kwa wimbo huu, lakini pia

wanapata tafakuri ambayo huwajenga watoto kuwa na vipawa vya juu katika kuchanganua mambo katika maisha halisi wanayoishi. Aidha, ucheshi pia unajitokeza katika nyimbo za kizazi kipya. Kutokana na matumizi ya ucheshi ndani ya muziki wa kizazi kipya watoto wanashajihika kuimba nyimbo za kizazi kipya zaidi kuliko zile nyimbo zao halisi. Hii inasababishwa na ucheshi katika nyimbo za kizazi kipya huambatana na ala za muziki. Kwa hivyo, huona wanaburudika zaidi kuliko katika nyimbo zao. Kwa ujumla, nyimbo za kizazi kipya hazina nafasi kubwa ya kuwajenga watoto kiakili katika kufikiri na kugundua mambo kama ilivyo katika nyimbo za watoto. Hayo yamethibitishwa na mtafitiwa ambapo alitoa mfano wa wimbo ufuatao ambao umeimbwa na msanii maarufu anaejulikana kwa jina la Ferouz.

Leo kuna mambo hadi soo mambo
asie na mwana abebe ndoo
Mikono juu, mikono juu oooo,
oye yee, oyaa mauwa oye yee
Tiririka, tiririka ivi natiririka ivi,
sharobaro kakatiza mitaa ya Tandika
Anapiga misere huku ametundika,
mradi watoto wa kitaa wanatawaga
Na mke wangu atababaika na kushobokea,
anacheza kichonchoroni
Masela wanampatanisha kimoja kimoja
wakaanaza kumpukutisha
Na wakasaula kila kitu
wakamuacha mtupu kabisa kama alivyozaliwa
Yaani mtupu kabisa
Oooo masela oya oya
Eeeee raia oya oya
Kama hajapinga mwanangu kama hajapinga
Oya oya, aaaaaaaa
Kama ndege mtini tunapendana
Sare sare kama shuleni tunaendana
Hatukeketani kama jeshini tunapatana
Hatukeketani kama vitani mama aaaa
Aiya iya ooo mama,aiya iya oo mama
Mikono juu, mikono juu chimba chimba
siri imeisha pochooo
Wape wazee wa vigodoro

hii ni kwa niaba yao
Sikia hii ni sauti ya Mgana IZE
kutoka East Africa big dancer
Wape mambo ya kishujaa
Katarina njoo mvua isinyeshe
Wamsegejuuu
Mzee na msoga utauona leo
Wazaramo mtanijua leo
Zenj Tabora mtaniona leo
Tanga Musoma mtaniona leo
Darisalama mtaniona leo
Wowo, wowo leo
Natamani niwe nao karibu
Nikila niwe nao karibu
Nikifurahi niwe nao karibu
Nitakutibu nukilala niwe nao karibu
ooooo,wow o wo leo
Watoto wa madaba punguzeni kukaba
Sharifu anajishauwa shauwa kikahaba
Chezea kiboda boda
T.M.K cheza kiboda boda
Ilala na kino cheza kiboda boda
Pancho Latino cheza kiboda boda
K Baa cheza kiboda boda
Zenj Kilimani KD aaaa
DJ Ibra cheza kiboda boda
Wazizo kwa madimba cheza kiboda boda
Espeni na Abuja cheza kiboda boda
Mzembe katembea kazembea

***Chanzo: kijana wa mtaa wa mkunazini, tarehe, 14/2/2015***

Msanii wa nyimbo hii katumia maneno mengi yenye maana ila katumia ucheshi ndani yake, kwa mfano, *hatukeketani kama jeshini* haina maana kwamba watu jeshini wanakeketana ila alitaka watu wafurahi tu kidogo wanapoisikiliza nyimbo hii, au aliposema *sare sare kama shuleni*, kama ndege mtini na mengineyo. Mtafiti alielezwa katika mahojianao na watafitiwa wake kuwa, ucheshi pia hujitokeza katika hali ya kujenga kiwiliwili. Watoto katika nyimbo zao hutumia viungo vyao kwa kuvichezesha ili kujiburudisha lakini kwa undani bila ya watoto wenyewe

kujifahamu, kuwa ni zoezi la kujenga mwili. Mhojiwa alitoa mfano wa wimbo ambao unaonesha zoezi la kujenga mwili. Mfano wa wimbo huo ni,

Marijani marijani marijani mtoto
Nilikwenda kisimani marijani mtoto
Nikakikuta kidege marijani mtoto
Kinaimba solomama ee solomama
Solomama eee solomama solomama

***Chanzo: Mwanafunzi wa darasa la nne Skuli ya Darajani, tarehe 12/2/2015***

Wimbo huu huimbwa na kikundi cha watoto wa kike wakiwa wamesimama, huanza kuimba taratibu huku wakipiga kofi kuanzia mwanzo wa wimbo hadi wanapofikia pale wanaposema wanaimba *solomama* huweka vidole juu ya kichwa na kiunoni na wakati huo huo wanazungusha viuno vyao.

Aidha, watafitiwa walieleza kuwa uwasilishaji wa nyimbo mbalimbali za watoto umeathiriwa na nyimbo za wasanii wa kizazi kipya. Athari ya mmomonyoko wa maadili ya watoto hujitokeza, kwani, watoto hujipa majina ya wasanii mbalimbali, pia, huiga mwendo, mavazi, mitindo ya ukataji wa nywele na usemaji, hali ambayo inawasababisha watoto waanze kuonekana kushusha suruali zao na hata kujishika sehemu zao za mbele na kurukaruka kama wasanii wa kizazi kipya.

#### 4.1.2.3 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Dhima

Kutokana na mahojiano na watafitiwa wameeleza kuwa, maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano yamechangia sana katika kuathiri dhima za nyimbo za watoto. Kama ambavyo imejitokeza katika uwasilishaji wa data, nyimbo za watoto dhima yake kubwa ni kuburudisha, kuelimisha, kushajihisha na kujenga mwili, lakini wasanii wengi wa muziki wameonekana kutumia mbinu ya mapenzi kwenye

nyimbo zao. Wimbo wa ***Nibemende*** wa muimbaji huyo mtoto anaejulikana kwa jina la Dogo Aslay umeonekana kuathiriwa na uimbaji wa wasanii wa kizazi kipya nchini Tanzania ambao hutumia mapenzi hii ili kuvuta soko la wasikilizaji na wanunuzi wa nyimbo zao. Haya yameelezwa na mtangazaji na mtayarishaji wa kipindi cha vijana na muziki kinachorushwa hewani kila siku ya Alkhamis jioni na shirika la utangazaji la Zanzibar (Z.B.C.T.V), anaejulikana kwa jina la Aunty Sophy. Mfano wa wimbo;

Ya moto, ya moto Band
Uuuu yeeee
Ya moto, ya moto Band
Mkubwa na wanawe
Kazini niende nirudi na sembe robo
Nnachotaka unipende nipunguze wenge kidogo
Waepuke wapambe wasilete mbwembwe uongo
Kwa maneno ya wembe wakatiana ngebe fujo
Moyo wa chuma sinaaa usije nipa tabu
Ongeza penzi kwa kina jumulisha na wivu
Achana nao wanaopiga majungu
Skendo mpya mi natoka na muzungu
Nipende mimi wengine kwako wachungu
Tumetoka mbali ugali na kalusungu
Nasema nibemende nipelembe nnachotaka si yetu yasonge
Waache wapige kelele ya kwetu sie yaende
Najuta ukiondokaaa najuta ongeza silaha baba na mama wakupende
Najutaa kaa na mimi na wewe wengine waende
Usijibanebane
Usijibanebane
Usijibanebane
Usijibanebane
Nakupa chnasi mama ya kuniperemba
Fanya vyovyote mimi nitapenda
Mtu kunywa kunywa milenda sio ufala ila kupenda
Nzi kufa kwenye kidonda sio ufala ila kupenda
Kaa mbali nami nimeshapenda
Kaa mbali nami nimeshapenda
Kaa mbali name kama kibaka
Nitie kwenye difenda
Kaa mbali name nimeshakufa
Kaa mbali name nimeshaoza
Kaa mbali name kama kibaka
Nitie kwenye difenda
Beibi,beibi nakupenda sana
Nishike nikushike milele tusije kuachana

Baki na mimi mimi
Wengine wa nini nini
Naogopa maradhi ndio mana niko makiiini mimi
How come nimezaliwa vipi
Vya utamu vimezaliwa vingi

***Chanzo: Mtayarishaji wa kipindi cha vijana na muziki Z.B.C.T.V.***

Ukiangalia umri wa mtoto aliyeimba wimbo huo haikumstahikia kwa mtoto kuimba hivyo ila ni zile athari ambazo zimeshaongelewa kwamba wasanii wa kizazi kipya wananguvu za kuwabadilisha watoto hawa kutoka mtazamo mmoja kwenda mwingine.

Vile vile, athari ya nyimbo za mapenzi zinazorushwa hewani na vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini zimeathiri nyimbo za watoto, kwani, watoto nao wanatumia fursa hiyo kutunga nyimbo zao zenye mwelekeo wa kimapenzi bila ya kudhani kuwa kufanya hivyo kunaziathiri nyimbo zao hizo. Mfano;

Kama dada wanipenda
Kaninunulie zeze
Nikilala kitandani
Zeze linibembeleze
Mama nalia
Kusema sema kubaya
Utamsema mkweo
Alokuzalia mumeo
Kadikanya kadikanya kadi
Namuogopa Ali
Kadi kanya kadi kanya
Atanilaza chali
Kadikanya kadi kanya
Katikati ya bahari
Namuogopa Juma
Atanipiga chuma

***Chanzo: Watoto michezoni mwao, tarehe, 9/2/2015***

Nyimbo hii inaimbwa na watoto wanapokuwa michezoni mwao lakini athari ya teknolojia ya habari na mawasiliano imeonekana kuiathiri nyimbo hiyo hata wazazi wakawa wanagomba watoto wao pindi wanapowasikia wanauimba wimbo huo kwani unakiuka maadili ya watoto.

Aidha, matumizi ya mapenzi hufanywa na wasanii ambao hueleza hisia zao za kimapenzi juu ya mtu fulani, au kuonesha jinsi walivyosalitiwa na wapenzi wao kwa kuwasifia au kuonesha malalamiko yao yanayohusu mapenzi. Wasanii wengi hutumia mbinu hii mfano, Banana Zoro katika wimbo wake wa ***Presha*** aliouimba na msanii Hafsa Kazinja ulikuwa ni wa majibizano ambayo mmoja alikuwa analalamika ni jinsi gani mpenzi wake anavyomsaliti, hadi kufikia kupata Presha, hayo yalielezwa na mtayarishaji wa kipindi cha watoto shirika la utangazaji Zanzibar (Z.B.C.Radio), (Fatma Moh'd, tarehe, 6/2/2015). Athari za muziki wa kizazi kipya katika nyimbo za watoto waishio mijini, zinatokana na kuenea kwa maendeleo ya sayansi na teknolojia, hasa teknolojia ya habari na mawasiliano katika wimbo huu. Athari zake zimeonekana hasa katika matumizi ya lugha, mahadhi na mtindo wa uimbaji. Kwa hivyo, kutokana na mjadala huo maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano, yameathiri kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa nyimbo za watoto katika uwasilishwaji na upokeaji wa dhima. Maendeleo hayo yamechangia mporomoko wa maadili katika jamii ya Wazanzibari, sio tu waishio mijini bali hata na vijijini. Maendeleo ya habari na mawasiliano yameifanya sanaa ya nyimbo za watoto kupunguza au kupoteza kabisa mantiki ya dhima zilizokusudiwa kuwasilishwa katika ujenzi na uimarishaji wa makuzi ya watoto kiakili na kiwiliwili.

Maudhui ya nyimbo za watoto waishio mijini, yameonekana pia kuathiriwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia hususan teknolojia ya habari na mawasiliano.

Katika kuzichunguza nyimbo hizo, mtafiti ameweza kubaini dhana mbalimbali ambazo zimejitokeza katika nyimbo ambazo ameweza kuzichunguza katika utafiti wake.

Kuburudisha ni miongoni mwa dhima ambayo imetolewa na watafitiwa katika nyimbo za watoto. Vile vile, nyimbo nyingi wanazoimba watoto wa mijini, zimeathiriwa na sayansi na teknolojia. Kutokana na kuiga na kufuata mtindo na muundo wa kuibua dhamira katika mtindo unaojitokeza katika nyimbo wanazozisikia katika vyombo vya habari. Nyimbo nyingi ambazo mtafiti amezichunguza zimeonekana kuwa na athari na dhima ya kuburudisha. Mfano wa wimbo huo ni ***Hodi na Karibu***. Matini ya wimbo wenyewe ni;

Hodi na karibu, hodi na karibu
Zamani tulifanya
Chagua mwenzako, chagua mwenzako
Zamani tulifanya
Umpeleke mbali, umpeleke mbali
Zamani tulifanya
Umrejeshe kwao, umrejeshe kwao
Zamani tulifanya
Mwambie kwa heri, mwambie kwa heri
Zamani tulifanya

***Chanzo: Watoto wa mtaani, tarehe, 13/2/2015***

Wimbo huu mara nyingi huimbwa na watoto wa kike na kiume. Watoto hao hujipanga katika mistari miwili moja ya kike na moja ya kiume. Wakati wa kuchezwa mchezo huu mwimbaji huanza kwa kuimba huo wimbo na mmoja mmoja hutoka kufuata maelekezo ya hiyo nyimbo mpaka wanapomalizika watoto wote kwa mpangilio huo. Kupitia wimbo huu, watoto hupata burudani ya kutosha hasa pale wanapochaguana na kufanya matembezi mafupi kabla ya kuamrishwa kumrejesha mwenzake.

Vile vile, wimbo wa ***Hodi na Karibu*** mbali ya kutoa burudani lakini pia huonesha dhamira ya upendo, umoja na ushirikiano kwani unapoambiwa uchaguwe mwenzako huwa tayari una mapenzi na yule unayemchagua, aidha utakuwa umevutiwa na tabia zake au jinsi anavyoonekana katika shughuli zenu mnapokuwa michezoni kama vile ukakamavu, mchapa kazi, mstaarabu na kigezo chema cha kuigwa.

Watafitiwa pia, wamemuelezea mtafiti ya kuwa nyimbo za watoto ukizichunguza kwa undani zinatoa taaluma ya kutosha. Ndani ya nyimbo hizo, watoto hupata kujifunza mambo mbalimbali wanayoyajua na wasiyoyajua. Kwa vile nyimbo za watoto ni moja kati ya aina ya fasihi simulizi, huenda na wakati na kubadilika kulingana na matukio. Pia, kwa vile dunia yetu sasa imo katika mabadiliko ya sayansi na teknolojia, nyimbo hizo nazo zimekumbwa na mabadiliko hayo. Watoto badala ya kuimba wimbo wa burudani tu wameona ipo haja ya kutunga nyimbo zinazokwenda na wakati na matukio yanayojitokeza kila siku hapa nchini. Matukio hayo wanayapata kupitia taarifa wazipatazo kupitia vyombo vya habari na mawasiliano. Mfano wa wimbo wa watoto wenye kuelimisha ni;

Sisi watoto wazuri
Tunasoma skuli
Tunapotoka shuleni
Tukimbilie nyumbani
Tusicheze majiani
Pamoja na misingini
Tusikubali kuitwa
Kupewa pipi na pesa
Njiani kuna vibaka
Hatari watatubaka
Hatudanganyikiiiiiiiiiii

***Chanzo: Watoto wa Skuli ya Darajani, tarehe, 12/2/2015***

Wimbo huu inawafunza watoto wasirande ovyo majiani wakati wanapotoka skuli au madrassa, kwa sababu kuna vitu vingi vinavyohatarisha usalama wao, kama vile maradhi ya miripuko na mafuriko pindi mvua zinaponyesha. Msisitizo huu umeonekana pale waliposema "tusicheze majiani pamoja na misingini", ili kuepuka ajali za barabarani na kuburuzwa na maji machafu. Pia watoto wanatahadharishana kuepuka tamaa ya kudanganywa na watu wasiowajua kwa kuwapa vitu kama vile pipi, pesa, chipsi na mingineyo na baadaye kuwafanyia vitendo vya udhalilishaji.

Wakati wa mwendelezo wa mahojiano mtafiti ameelezwa kwamba baadhi ya wasanii wa kizazi kipya, huimba nyimbo zenye kuielimisha jamii kutokana na kuwepo kwa majanga mbalimbali kama vile maradhi, ubadhirifu wa mali za umma, rushwa na mingine mingi. Msanii maarufu wa kizazi kipya Feruzi alitoa wimbo unaoitwa ***Starehe*** kipindi ambacho maradhi ya ukimwi yameshamiri nchini petu. Alitumia wimbo kuwaelimisha watu athari za kuendekeza ngono na starehe zisizokuwa na mpaka, kwani mwisho wake ni majuto. Feruzi alifanya hivyo kwani alijua kwamba watu wengi wanasikiliza nyimbo hivyo ujumbe ungepatikana kwa urahisi. Mfano wa wimbo ni huu ufuatao;

Hapa nilipo mimi nipo kitandani
Starehe zimeniweka matatani
Kupona tena mimi haiwezekani
Masela wangu ndugu zangu buriani
Kwaherini, kwaherini, kwaherini
Bongo ree na majaji kwaherini
Hamtoniona tena duniani
Sasa najuta mwenzenu yamenikuta
Ibilisi amefanikiwa kunivuta
Sasa sijui wa kumlaumu nani
Kati ya nafsi yangu ama shetani
Kwaherini, kwaherini, kwaherini
Makongo na jitaudi kwaherini,
Dar na Azania kwaherini aaaaaa
Saa saba juu ya alama nikiitazama
nishaachana na jaji

Sasa namfata salama, saa kumi na mbili
nakwenda na mademu wawili
Achana na yule niliekutana nae saa mbili,
demu wa Mikocheni sasa
Hayupo tena duniani nilikuwa
nikimsubiria pale maskani kijiweni
Amina na Semeni tunakutana
kwa Macheni na huko nilikuwa
Nabadilisha tena kwa foleni
Huo ndo ulokuwa mwenendo wa maisha yangu
mimi nilikuwa najivinjari na machangu
Aaaaaaa niliona fahariiiii yee
Starehe nilizifanyia papara nilibadili
mademu kama vidaladala nikipanda hii
Nikirudi ileeee nilitamani starehe zote nizitawale
hata kumkumbuka Mola wangu ilikuwa nadra
Kutembea na wasichana nilikubuhu
nilitembea na watoto wa geti hadi machangu
Ubaya kwamba kondom sikuitambua
nikahisi ladha ya mapenzi itapungua
Kumbe ilikuwa ninapotea njia
nililoambiwa mimi nilipuuzia
Idadi ya wanawake ikawa lukuki
ikafika kipindi siwakumbuki ona, onaaaa
Ona sasa yalonisibu kwa dadaake Bashiri
nishasahau kama tulishakutana kimwili
Nilipomuona nikamtongoza tenaaa
tena kwa mara ya pili ona sasa aaaaaaaa
Kijana vipi mbona hujagonga mlango
Jipange kwenye foleni mmoja mmoja ndio mpango
Ondoa mashaka tiba bora haitaki haraka
Subiri watibiwe wenzio na wewe zamu yako itafata
Dokta mimi nimekuja kufanya hitimisho
Na hii ndo itakuwa ndo ngwe yangu ya mwisho
Dalili zinaonesha nimeathirika
Nimekuja pima tu nipate uhakika
Hebu cheki dokta nilivyokonda
Mwili wote umekonda umebaki vidonda
Hii yote dalili ya umeme dalili ya umemeeeee
Homa za mara kwa mara kwangu hazishi
Kuharisha na kutapika mara sitini na tano kwa wiki
Hebu angalia hata nywele zilivyonyonyoka
Mabega yamepanda juu utadhani yanachomoka
Ninao ninao subiri kipimo
Ninao ninao usikate tamaa
Ninao ninao dokta usinipe moyo
ni sawa na mafupa kutafuna kibogoyo
Duniani mimi sina umuhimu kuiaga dunia
napaswa na inanilazimu

Ni bora tu nielekee kuzimuuu
No!no acha maamuzi
Na ni ulimbukeni kujiua pasipo sababu
Maradhi ni kawaida kwa binaadamu hilo ufahamu
Ni vyema ungetulia ukasubiri majibu
Dokta kwani mimi nasubiri nini
ni bora niwe wa kupumzika kaburini
Starehe mnazipenda ila mwisho wake mbaya
Wengi wameteketeya kwa kuendekeza umalaya
Vipimo vinaonesha ni kweli umeathirika
Aaaa I'm very sorry
Ni vyema kufanya ibada na kurudi kwa muumba wako
Kula vizuri, fanya mazoezi, pumzisha mwili wako,
Ukizingatia haya utaishi kwa matumaini
By the way unayo nafasi hebu jaribu.
Hata Muumba nimeshamkosea
Na mbingu zote zinanizomea
Hata Malaika wa adhabu kwa hamu wananingojea
Nikifika huko nani atanipokea aaaaaaaaa

***Chanzo: Mwalimu wa Skuli ya Darajani, tarehe, 12/2/2015***

Wimbo huu wa Ferouzi unaelimisha jamii kuacha starehe na zaidi kuacha ngono. Ameelimisha zaidi kuhusiana na gonjwa zima la ukimwi kama vile chanzo, dalili na athari za ukimwi ili watu wajiepushe nazo na kujitahidi kufanya ibada kwani mwisho wa starehe ni mbaya unaweza kupata maradhi mbalimbali ya kuambukiza. Nyimbo hizo waziimbazo katika michezo yao huwasaidia katika kuimarisha na kuwakuza kiakili. Ujuzi mwingi walionao watoto katika utambuzi wa kujua mambo unatokana na baadhi ya nyimbo ambazo watoto wanaziimba katika michezo yao. Nyimbo hizo huwafanya watoto wawe na udadisi zaidi. Kwa mfano; baadhi ya nyimbo waziimbazo watoto hujifunza kurithishana wao wenyewe toka kizazi kimoja hadi kingine.

#### 4.1.2.3 Athari za Sayansi na Teknolojia katika Uhifadhi

Katika mahojiano ya mtafiti na watafitiwa, mtafiti amebahatika kuelezwa kuwa, katika miaka hii nyimbo za watoto zimepoteza uasili wake, kwani hapo kabla nyimbo za watoto zilikuwa zikihifadhiwa katika vichwa na vifua vya watu, lakini mabadiliko ya maendeleo ya tasnia ya habari na teknolojia katika nyimbo za watoto yamesababisha kupungua ukuaji na maendeleo ya nyimbo hizo, kwani watoto wanaishia kuhifadhi na kuimba nyimbo wanazoziona na kuzisikia katika vyombo vya habari na mawasiliano.

Watafitiwa wamesema kwamba, tabia na mwenendo wa watoto katika kutunga na kuwasilisha nyimbo zao, kwa kiwango kikubwa, umeathiriwa na maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Idadi kubwa ya vyombo vya habari mjini kama vile televisheni na redio hupiga nyimbo mbalimbali za wasanii, hivyo, watoto huiga nyimbo za wasanii ambazo huzisikia zikipigwa katika vyombo hivyo. Kwa mfano, wimbo wa Mbagala ulioimbwa na msanii Diamond, watoto wameathirika na wimbo huo na kutunga wimbo wao wenye mapigo yenye kufanana na wimbo wa huo ambao unaimbika kama unavyoonekana hapo chini.

Tatizo kwetu tauniiii
Mchana wali juisi ya pesheniiiii
Jioni tunakula koniiiii
Usiku kujirusha viwanjaniiiii
Tatizo kwetu tauniiiii
Kuishi ng’ambu mi siweeeezi

***Chanzo: Mwanafunzi wa skuli ya Mkunazini, tarehe, 13/2/2015***

Wimbo huu wenye mahadhi ya wimbo wa kizazi kipya Mbagala uliimbwa na watoto wakati mtafiti alipotaka kuona vipaji vyao vya utungaji wa nyimbo mbalimbali katika skuli ya Mkunazini.

Kwa kawaida tabia na mwenendo wa kuhifadhi nyimbo za watoto katika mikanda ya vinasa sauti, santuri, CD au DVD havikuwepo kabla ya maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

Katika utafiti huu, mtafiti ameweza kupata nyimbo za watoto hawa waishio mijini zikiwa zimehifadhiwa katika CD. Nyimbo hizo zikiwa zimehifadhiwa na ZBC redio na televisheni, pia mashuleni kwenye sherehe mbalimbali za mahafali ambazo hufanyika kila mwaka.

Katika kutafuta data, mtafiti amepewa CD hiyo na uongozi husika na kuweza kubaini ni jinsi gani teknolojia ilivyoathiri uhifadhi na matumizi ya nyimbo za watoto. Baada ya kuziangalia CD kwa kina mtafiti alimhoji mtafitiwa kwa kumuuliza kuwa, wanahisi hakuna athari yeyote ya kuhifadhi nyimbo za watoto katika vinasa sauti na picha? Watafitiwa wamekiri kuwepo kwa athari, lakini wametetea kuhifadhi kwa njia ya vyombo vya teknolojia ni bora kwani nyimbo hizo zitadumu kwa muda mrefu na kubahatika kuimbwa na kusomwa na vizazi vingi, lakini kama nyimbo hizo zitabakia vichwani na vifuani mwa watu zitapotea na kufa kama wanavyokufa binaadamu. Ila wahojiwa pia wamekubali swali la kuporomoka kwa maadili, lakini hali hiyo inasababishwa na utukutu na udadisi wa watoto katika kutaka kujua mambo kwa haraka.

Licha ya nyimbo za watoto ambazo ni za asili zinazowasilishwa kwa mdomo huku fanani na hadhira wakiwa wanaonana ana kwa ana, hivi sasa kumeibuka nyimbo za watoto lakini zinawasilishwa kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano

### 4.1.3 Mchango wa Sayansi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa Nyimbo za Watoto Waishio Mjini Zanzibar

Maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa nyimbo za watoto waishio mjini Zanzibar yamekuwa na kuenea kwa kiasi kikubwa katika kipengele cha uwasilishaji, dhima na uhifadhi. Mchango huo ni kama ufuatao ulioelezwa na watafitiwa.

#### 4.1.3.1 Uwasilishaji

Uwasilishaji wa nyimbo za watoto kabla ya maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano mjini Zanzibar yalikuwa ni ya ana kwa ana. Watoto walikuwa wanajikusanya pamoja aghlabu, nyakati za usiku wakiimba nyimbo zao zenye kuambatana na michezo tofauti.

Watafitiwa wameeleza kuwa, muundo wa nyimbo za watoto haukuwa na mtindo maalumu wa uwasilishaji bali hutegemea aina ya wimbo wenyewe. Ziko nyimbo ambazo huimbwa na watoto wawili na zile zenye kutumia mkusanyiko wa watoto. Wimbo kama vile ***Shuwadina*** ulikuwa unaimbwa na watoto wawili tu lakini ***Ukuti, Hodi na Karibu*** na nyinginezo zilihitaji watoto wengi ambao hufanya wimbo huo unoge. Nyimbo hizi mara nyingi zilitofautiana baina ya sehemu moja na nyengine. Hali hiyo, inasababisha kuonekana wimbo wa aina moja ambao unatofauti ndogo ndogo za kilugha, mtindo wa uchezaji au aina ya wahusika kutokana na mila na utamaduni wa jamii husika. Mfano, picha namba 4.2 watoto wakicheza mchezo wa nyimbo ya ***Hodi na Karibu.***



**Picha 2: Watoto wa Skuli ya Darajani wakicheza na kuimba wimbo wa Hodi na Karibu, (chanzo mtafiti 18/2/2015)**

Aidha, watafitiwa wamedai kwamba baada ya maendeleo ya teknolojia na mawasiliano kushamiri, nyimbo nyingi walizokuwa wakiimba watoto zimekuwa za aina moja, kwani watoto kwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari huona, husoma na kusikia nyimbo ambazo huimbwa na watoto wenzao wa sehemu nyingine. Kwa hivyo, kwa vile watoto ni wepesi kuiga, hivyo, huchukua muundo, mtindo na kutumia lugha inayotumika katika jamii fulani. Pia, wamesema kuwa watoto huimba nyimbo zenye mchanganyiko wa lugha, hivyo, watoto hukariri maneno yaliyomo kwenye nyimbo mbalimbali zinazorushwa hewani na vyombo vya habari hatimaye kuyazowea maneno yaliyotumika katika nyimbo hizo. Hivyo, huongeza misamiati zaidi katika lugha yao kwa maana hiyo, lugha hukua.

Vile vile, kutokana na maelezo ya watafitiwa lugha ambazo hutumiwa na wasanii, nazo watoto wanapozisikia huwa ni wepesi wa kuzifahamu na kuzitumia kwa mfano; msanii maarufu na mkongwe Dully Sykes maarufu kwa jina la Mister Misifa

katika tasnia ya muziki aliimba wimbo wake wa ***Nyambizi.*** Neno hili lilitumika kama jina la wimbo tu ila baadaye likawa kama msamiati unaoashiria Ukimwi. Pia watoto hupata kujifunza mitindo mbalimbali ya uchezaji na uimbaji wa nyimbo zao kama vile kuchanganya lugha pamoja na kucheza kwa kujinengua na kujishika viuno.

Baadhi ya wahojiwa wameeleza kuwa maendeleo ya teknolojia ya habari yamechangia katika usambazaji na ueneaji wa nyimbo za watoto. Kwani nyimbo hizo husikilikana sehemu za ndani na nje ya Zanzibar halikadhalika, wasanii huzitumia kupitia nyimbo zao mbalimbali na kuzifanya zienee kwa haraka zaidi, mfano, wimbo wa ***Kinyulinyulika*** ambao asili yake ni wimbo wa watoto lakini pia msanii anaejulikana kwa jina la Sameer ameutumia katika wimbo wake unaoitwa ***Kinyulinyuli.***

Katika kipengele cha uwasilishaji pia wahojiwa wameeleza kuwa nyimbo za watoto kutumiwa na vyombo vya habari imesaidia kuibua vipaji na vipawa vya watoto. Watafitiwa wameeleza kuwa kabla ya maendeleo ya habari na mawasiliano, watoto walikuwa wamedumaa katika uibaji na uwasilishaji wa nyimbo zao kwa mujibu wa mazingira yao wanayoishi. Watoto walikuwa wakiimba nyimbo hizo hizo ambazo zinaelimisha na kushajihisha jamii yao tu, lakini baada ya maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano watoto wameweza kuona nyimbo mbalimbali za watoto wenzao zikiimbwa kutoka sehemu tofauti ulimwenguni hali ambayo imewasababisha na watoto wa mjini Zanzibar kubadilika taratibu katika uwasilishaji wa nyimbo.

Aidha, watafitiwa wamezidi kusisitiza kuwa, maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano yamesaidia sana kuisambaza sanaa ya nyimbo za watoto waishio mjini

Zanzibar, kwani, vyombo hivyo viliandaa vipindi mbalimbali vinavyohusisha michezo, nyimbo na hadithi za watoto. Kwa hivyo, matokeo hayo yanaonesha mchango wa maendeleo ya habari na teknolojia kwani kabla ya maendeleo hayo sanaa hii ya nyimbo za watoto haikuweza kurushwa hewani, na watoto kuweza kuona vipaji vya watoto wenzao wa sehemu nyingine.

#### 4.1.3.2 Dhima

Katika mchakato wa uchambuzi wa dodoso ndogo za watafitiwa, imepatikana jawabu kuwa, miongoni mwa mchango wa teknolojia ya habari na mawasiliano kwa nyimbo za watoto ni kuibua vipaji. Vipaji hivyo baadaye huwawezesha watoto kujitegemea kiajira. Watoto wanapoimba kwa kutumia vyombo vya habari huonekana na kusikilikana sehemu mbalimbali za ulimwengu. Hivyo, baadhi ya watoto huvutiwa na uimbaji wa watoto wengine na hatimaye kuibuka baadhi ya wadau kuwadhamini watoto hao na kuwaendeleza vipaji vyao. Watoto hao wanapokuwa na kujiona hawana ajira hujitumbukiza katika uimbaji kwani tayari kipaji ameshakuwa anacho, kwa vile ni mzoefu wa kuimba nyimbo za watoto huwa makini na kujiamini anapoimba mbele ya hadhira. Mfano mzuri ni msanii Dogo Aslay alianza kuimba utotoni hadi sasa amekuwa ni mwimbaji maarufu hapa nchini Tanzania.

Vile vile, imeelezwa kuwa vyombo hivyo vya habari vinasaidia kutoa taaluma ya kutosha kwa jamii ya watoto na hata watu wazima dhidi ya matukio na majanga yanayotokea mjini Zanzibar, pamoja na ulimwenguni kote. Taaluma mbalimbali zinazohusu maradhi, vita, na kama vile ubakaji husikika na kuonekana kupitia vyombo hivyo vya habari. Mambo hayo huwasilishwa kwa kupitia nyimbo za watoto.

Halikadhalika, wahojiwa wameeleza kuwa, teknolojia ya habari na mawasiliano imechangia katika kuibadilisha jamii kimaendeleo kutokana na dhamira zinazoibuliwa kwa kupitia nyimbo za watoto zinazorushwa hewani. Kwa vile, jamii ya watoto inapokea kwa kuzisikia nyimbo za watoto wenzao kutoka sehemu tofauti, zinawajenga watoto hao katika hali ya kubadilika kimtazamo wa kimaendeleo. Kwa mfano, jamii inaweza kuachana na mila ya ukeketaji na ajira za watoto kutokana na wimbo waliousikia kwa kupitia vyombo vya habari na mawasiliano. Aidha, watoto huweza kubadilika katika uwasilishaji wa nyimbo zao katika muundo, mtindo na lugha kwa sababu ya kuona kwa kiasi gani jamii ya watoto wenzao wameshaendelea katika michezo ya watoto. Kwa hivyo, wahojiwa wamelitilia mkazo swala la maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano ni chombo chenye kuleta msukumo na maendeleo ya haraka ya nyimbo za watoto.

#### 4.1.3.3 Uhifadhi

Mchango mwingine wa teknolojia ya habari na mawsiliano kwa nyimbo za watoto waishio mjini Zanzibar, ambao umeelezwa na watafitiwa ni kwamba kabla ya maendeleo hayo nyimbo za watoto zilikuwa zikihifadhiwa katika vifua vya watu na kurithishana kutoka kizazi hadi kizazi. Uwepo wa nyimbo hizo ulikuwa ni pale tu ambapo mwenye kuhifadhi nyimbo yuhai ama yupo na si vinginevyo yaani inawezekana kufa au kusahau kwake ndio kufa au kupotea kwa fasihi hiyo. Mara baada ya teknolojia ya habari na mawasiliano kuenea mjini Zanzibar, watu walianza kuacha utaratibu wa uhifadhi wa nyimbo zao na kuanza kujiingiza katika mkumbo wa kurikodi nyimbo za watoto kupitia vitabu mbalimbali, majarida, mikanda ya video, santuri, DVD na VCD. Msukumo huo uliwezesha hata zile nyimbo za zamani za watoto za asili zikianza kurikodiwa na vyombo vya habari kama zilivyo katika

uhalisia wake. Kwa mujibu wa maelezo ya mtayarishaji wa vipindi vya watoto Riziki Stanley (Anti Iki) alisema:

> "Sisi tuna utaratibu wa kutembea vijiji hadi vijiji na kuwatembelea watoto wa shule kuandaa vipindi vya watoto. Watoto huwa tunawaimbisha, wanatoa hadithi, vitendawili na hata maswali ya kuchemsha bongo. Vile vile, siku za sikukuu huwa tunawaalika watoto wadogo kama vile chekechea hadi darasa la tatu kusherehekea sikukuu pamoja kwa vipindi vya redio na televisheni, watoto hao huburudika kwa kuimba nyimbo, kutoa hadithi na vitendawili", (Anti Iki, 16/2/2015).

Kwa hivyo, kwa mujibu wa mchango wa maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano na kama mfano wa maelezo yaliyotolewa na mtayarishaji wa kipindi (mtafitiwa), uhifadhi wa kutumia vyombo hivyo umesaidia sana kwani utaifanya sanaa ya nyimbo za watoto kudumu kwa muda mrefu. Uhifadhi na uthabiti wa nyimbo za watoto waishio mijini katika muktadha wa maendeleo ya habari na mawasiliano umeweza kusaidia katika kuhifadhi vizuri nyimbo za watoto kuliko ilivyofikiriwa na wanamapokeo.Uthabiti wake ni wa kudumu, kwani leo hii nyimbo nyingi zinawekwa kwenye vifaa mbalimbali kama vile kompyuta, (flopy/flash), mikanda ya santuri na video au katika CD. Hivyo nyimbo zinakuwa zinaendelea kuwepo kwa muda mrefu sana sawa na fasihi andishi inavyokuwa inahifadhiwa katika maandishi. Kwa upande wa video uhifadhi wake huendelea kuonesha vitendo na sauti na huweza kudumu hata zaidi ya maandishi kama zitatumiwa vizuri.

## 4.2 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amewasilisha na kujadili namna teknolojia ya habari na mawasiliano ilivyoathiri nyimbo za watoto waishio mijini. Katika kuchunguza nyimbo za watoto hawa waishio mijini, katika kuwepo vyombo vya habari na mawasiliano, vimeonekana kuathiri kwa kiasi kikubwa sana nyimbo za watoto

katika fani na maudhui yake. Kwa jumla lengo la kuvichunguza na kuvibainisha vipengele vyote hivyo, vilivyojadiliwa ni kutaka kuonesha jinsi maendeleo haya yanavyoathiri nyimbo za watoto waishio mijini pia kueleza mchango wa vyombo hivyo kwa sanaa ya nyimbo za watoto waishio mjini Zanzibar. Sura inayofuata imezungumzia hitimisho la tasnifu pamoja na mapendekezo ya mtafiti kwa utafiti huu na zijazo.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza mambo mawili makuu. Jambo la kwanza ni hitimisho la taarifa za utafiti huu kwa muhtasari. Jambo la pili inaelezea mapendekezo yanayowasilishwa kufuatia matokeo ya utafiti huu.

## 5.2 Hitimisho

Matokeo ya utafiti huu yameweza kujibu maswali ya malengo ya utafiti huu kwa kuzingatia nadharia ya Usosholojia. Pamoja na kuwa utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi teknolojia ya habari na mawasiliano ilivyoathiri nyimbo za watoto waishio mijini, mtafiti amefanikiwa kupata majibu yaliyoongoza utafiti huu. Kutokana na utafiti huu, mtafiti ameweza kubaini kuwa, nyimbo za michezo ya watoto zinapotea kwa kiasi kikubwa sana na badala yake teknolojia ya habari na mawasiliano inachukua nafasi kwa kurusha nyimbo mbalimbali za wasanii chipukizi, ambazo zinaonekana kupendwa zaidi na watoto kuliko nyimbo zinazowahusu kama watoto. Hayo yaliweza kubainika kwa kuanzia na kujibu swali la kwanza ambalo lilikuwa linataka historia ya nyimbo za watoto Zanzibar.

Pia utafiti huu umebaini kuwa teknolojia ya habari na mawasiliano imekuwa chachu ya kuhifadhi nyimbo za watoto zisizidi kupotea ingawa zinapoteza uwasili wake. Miongoni mwa athari zilizobainishwa ni kuporomoka kwa maadili ya jamii hususan, kwa vijana ambao ndio taifa tegemezi la jamii, badala yake kuiga mila na silka za jamii nyingine.

Pia utafiti huu umebaini kuwa wasanii wengi hupenda kuzitumia nyimbo za watoto kwenye nyimbo zao ili kuongeza ladha ya nyimbo hizo na kuongeza soko la wasikilizaji na wanunuzi wa kazi zao hivyo, kuwafanya watoto wawapende na kuzipenda zaidi nyimbo hizo kuliko nyimbo zao. Aidha, utafiti huu umegusia mchango wa teknolojia ya habari na mawasiliano kwa nyimbo za watoto waishio mjini Zanzibar na kubaini kwa kiasi gani zinasaidia maendeleo ya nyimbo hizo.

Matokeo ya utafiti huu yanathibitisha kauli ya nadharia inayoongoza utafiti huu. Ni ukweli usiopingika kwamba nyimbo za watoto kama ni kazi ya fasihi simulizi inahusishwa na mazingira ambayo inaizunguka jamii, jamii ambayo hukumbwa na mabadiliko ya aina mbalimbali ambayo huhusisha kukua kwa maendeleo kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Kazi hii inatekeleza matakwa ya jamii kwa namna tofauti. Mihimili ya nadharia kuhusu kazi hii ya fasihi simulizi (nyimbo za watoto na uwendelezwaji wake zinaweza kuonekana kwa kuangalia uwasilishwaji wake pamoja na kutumika kwake katika jamii. Aidha utendaji kazi wake umebainika kupitia nyimbo mbalimbali zilizochunguzwa na mtafiti.

**5.3 Mapendekezo**

Utafiti huu umegundua umuhimu mkubwa uliopo katika kuendeleza nyimbo za watoto ambazo zimebainika kupotea siku hadi siku. Kutokana na hali hiyo, Mapendekezo yafuatayo yamezingatiwa;

-Kuna haja ya kuingiza nyimbo za watoto kwenye mitaala ya shule ili zisipotee.

-Jamii ione umuhimu wa nyimbo za watoto kwamba mbali ya burudani nyimbo za watoto huwapatia mazoezi tosha ya viungo hivyo kuwafanya watoto wachangamke.

-Kuna haja ya kuendeleza tafiti zaidi ili kubaini dhana muhimu kama vile istilahi/misamiati inayopatikana katika nyimbo za watoto ambazo bado hazijapatiwa maana zake.

-Asasi za kielimu zitilie mkazo somo la fasihi simulizi kwa kukifanyia kazi kipengele hiki cha nyimbo za watoto.

-Nyimbo za watoto ziandikwe kwa kufanyiwa uchambuzi zaidi.

-Jamii iwasaidie watoto katika kuwafundisha nyimbo zao ili zisije zikapotea zaidi

-Tafiti zaidi zinahitajika katika vipengele vya lugha ya nyimbo za watoto.

Kutokana na mapendekezo hayo ni wazi kuwa utekelezaji wa mapendekezo hayo utaondoa mapungufu yaliyopo.

### 5.4 Hitimisho

Sura ni imeelezea hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Katika maelezo hayo, zimeelezwa kwa muhtasari sura zote nne zilizotangulia. Aidha sura imetoa mapendekezo kuhusu utafiti huu na tafiti zijazo kuhusiana na mada ya utafiti huu.

## MAREJELEO

Amir, D. (1996), *Experiencing Music Therapy: Meaningful Moments in the Music Therapy Process.*

Bailey, L.M. (1994), *The Use of Songs in Music Therapy With Cancer Patients and Their Families*.

Balisidya, M.L. (1987), "Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi." Mulika 19:2-10.

Bukenya, A & Nadwa, A J 1983, *African Oral Literature*, Nairobi, Longmans. EC4P.

Finnegan, R 1970, *Oral Literature in Africa*, London & Nairobi, Oxford University Press.

Finnegan, R. (1970), *Oral Literature in Africa*, Oxford University Press. London.

Finnegan, R1977, *Oral Poetry Its Nature, Significance and Social Context*, Cambridge University Press, Cambridge

Finnegan, R1992, *Oral Tradition and Verbal Art A guide to Research Practice,* New fetter Lane, London.

Hamad, A. KH. (1982), *Tanzu za Fasihi Simulizi: katika TAKILUKI. Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. *Tanzania:* Publishing House. Dar es Salaam.

Hilaal, N. M. (2007), *Mfinyanzi Aingia Kasri. Siti Binti Saad*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publisher.

Juma, S. K. (2011), *Athari chanya na hasi za Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia katika Fasihi Simulizi,* Chuo Kikuu Cha Dodoma.

Kitundu, A. (2011), "Athari za Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia kwenye Fasihi Simulizi: Nyimbo za Ibada ya Dini ya Kikristo Tanzania; Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kombo, D. and Tromp, D. (2006), *Proposal and Thesis Writing; An Introduction*, Paulines Publications, Nairobi.

Kothari, C. (2004), *"Research Methodology, Methods and Techniques",* New Delhi, New Age International (p), Ltd.

Matteru, M. D. (1983), "Fasihi Simulizi na Uandishi wa Kiswahili, katika Fasihi": *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. UK 26-37.

Mbarouk, A. A. (1983), "Nyimbo za Michezo ya Watoto".in TAKILUKI, (editors), *Fasihi Simulizi Zanzibar*. TPH, Dar es Salaam, pg 47-65.

Mdowe, S. R.(2011), "Nyimbo za Michezo ya Watoto zinavyobadilika na wakati kifani na kimaudhui katika wilaya ya Magharibi Unguja". Chuo Kikuu cha Dodoma.

Miruka, O. (1994), *Encounter of oral literature*, East African Educational Publishers, Nairobi.

Mlacha, S.A.K. (1995), "Fasihi Simulizi na Usuli wa Historia ya Pemba". Katika: *Lugha Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI. Uk, 16-26.

Mwaje, J. I. (2006), *Back ground to social science Research Methodology*, Nairobi, Kenya.

Ockpewho, I. (2006), *African Oral Literature: Background,Character and Continuity Bloomington* Indiana

Ong, W. (1982), *Orality and Literacy*, Methuen, London.

Opie I, and Opie P, (1977), *The Oxford Dictionary of Nursery Rhymes*, Oxford University Press.

Simiyu, W. F. (2011), *Kitovu cha Fasihi Simulizi,* Serengeti Book Shop Mwanza.

Taban lo Liyong, (1972), *Popular Culture in East Africa*, Nairobi, Longman.

Wamitila, K.W. (2003), *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi*, Focus Publications Ltd, Nairobi.

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO 1

## HOJAJI NA MADODOSO YALIYOTUMIKA KUKUSANYA DATA ZA UTAFITI HUU

**a) Mwongozo wa Hojaji kwa Wazazi na Walezi wa Watoto Waishio Mijini**

1. Unaitwa nani?
2. Una miaka mingapi?
3. Je umeshawahi kusikia neno teknolojia ya habari na mawasiliano? Kama ndiyo eleza unavyoifahamu.
4. Historia ya nyimbo za watoto Zanzibar ikoje kabla na baada ya maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano?
5. a) Maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano yameathiri nyimbo za watoto?

   b) Kwa namna gani?
6. Kuna tofauti gani ya uwasilishwaji, dhima na uhifadhi kwa nyimbo za watoto kabla na baada ya maendeleo ya habari na mawasiliano? Eleza kwa ufupi.
7. Teknolojia ya habari na mawasiliano imetoa mchango gani kwa sanaa ya nyimbo za watoto kwa upande wa;

a) Uwasilishaji

b) Dhima

c) Uhifadhi

**b) Dodoso kwa Watoto Waishio Mijini katika Wilaya ya Mjini Magharibi.**

Jina la mtafiti Bimkubwa Abdulrahman Hemed

Tarehe ya kufanya udodosi 9/2/2015

Mahali pa kufanya utafiti

Utafiti huu unahusu athari za maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA) katika nyimbo za watoto.Tafadhali naomba ushirikiano wako katika kujibu maswali yafuatayo;

Weka alama ya ndio katika mabano () na toa maelezo mafupikatika sehemu zilizoachwa wazi.

1. Jina lako unaitwa nani?.................
2. Unasoma darasa la ngapi?

   Kwanza (), Pili (), Tatu (), Nne ()……………
3. Nyimbo za watoto ni zipi?
4. Nyimbo za watoto huimbwa vipi na wakati gani?
5. Uko wimbo wowote wa watoto unaoujua ambao umeusikia ukiimbwa redioni au katika televisheni? Umepata ujumbe gani kupitia wimbo huo?
6. Kwa nini watoto mnaimba?
7. Taja vyombo unavyovifahamu ambavyo vinatumika katika kutoa habari na burudani,hasa nyimbo.

i. ………………….

ii. ………………

iii. …………………..

iv. ……………………..

8. Orodhesha majina ya wasanii uwajuao pamoja na majina ya nyimbo walizoziimba.

i. ………………………….

ii. ……………………..

iii. ……………………………..

iv. ………………………………….

9. a) Kuna madhara yoyote yatokanayo na kusikiliza/kutazama nyimbo kwa muda mwingi kupitia vyombo vya habari kama televisheni/radio?

   Ndio ()                Hapana   ()

   b) Kama jibu ni ndiyo yataje madhara hayo yanayojitokeza katika nyimbo

   mziimbazo……………………………………………………………

   ……………………………………………………………………

…………………………………………………………………………

……………………………………………………………………..

10. Toa maoni yako ya jumla kuhusu maendeleo ya vyombo vya habari katika maendeleo ya nyimbo mziimbazo muwapo katika michezo mbalimbali.

…………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………

………………………………………….

## KIAMBATISHO 2

## NYIMBO ZA WASANII MBALIMBALI WA KIZAZI KIPYA.

**Samir : 1. *Kinyulinyuli***

Ni bora uwe mchoyo
Nisikufume kwenye kichochoro
Usiniweke kiporo
Ukajazua mgogoro
Nikupeleke nyashiro
Tukale wote ng'arambo
Kama klabu twende sansiro
Nitakupa sana mabaro
Kule utamu kunoga
Wenye radha kama bagaa
Wanasema umeniroga
Umenifanya ndondochaa
Mami wewe ni maji
Kwenye jangwaaa
Ifungue dibaji unisomeeee
Usinidengulie
Kinyuli nyuliii nyulika × 2
Kidali kikidali kidalipo × 2
Njoo tucheze kinyuli nyulii nyulika
Kinyuli nyuuulii nyulika

Sinyooritaaaa × 2
Kisuuuraaaa × 2
Usiruke ruke kama ndege
Chanda chema huvikwa pete
Jifungie ndani kama kobe
Wasije wakakunasaa
Wakavuja kama pakachaa
Usijitoe sadaka
Kwa tama ya nyama ya bata
Kinyuli nyuliii nyulika × 2
Kidali kikidali kidalipo × 2
Njoo tucheze kinyuli nyulii nyulika
Kinyuli nyuuulii nyulika

Seke seke la mapenzi
Linauma hatariii
Na mgonjwa wa mapenzi
Akipona akusii
Kama zoba mi bora niwe zoba
Huu mkuki na uniuwe
Mwenye chake sifatiliwe

Mji mwema hupigwa mawe
Kinyuli nyuliii nyulika × 2
Kidali kikidali × 2
Njoo tucheze kinyuli nyulii nyulika
Kinyuli nyuuulii nyulika
Kula tumbakishie baba × 2
Kula tumbakishie mama × 2

***Chanzo: Radio Zanzibar tarehe 15/2/2015***

**Mkubwa na wanawe: 2. *Nikupe Peti***

Mkubwa na wanaawe
Na wanaaawe
Macho yananiumiza roho
Silali tu nisipokuona nnaumia roho
Kwenye mapenzi hakunaga komandoo
Kuna popo wa mbali wanazimisi shoo
Nibusu nikubusu × 2
Nikupeeti Peeti chumbani × 2
Kukuacha sithubutuuu
Wewe wangu halaali mwandani
Kwenye joto nipeepee × 2
Ukichoka jilaze kifuani
Vumilia mabeibee
Tupatacho kidoogo afueni
Niu niuee mahaba niuweee
Wooo wow o woo hiki kisiki cha mpingo cha mpingo× 2
Wacha mwenzenu nicheke japo nna pengoo× 2

Wanavyokupiga majungu mwenzako natetemeka
Wasije Wachina Wazungu wakaja wakakutekaaa maama
Niu niuee mahaba niuweee
Kwenye joto nipeepee × 2
Ukichoka jilaze kifuani
Vumilia mabeibee
Tupatacho kidoogo afueni
Wooo wow o woo hiki kisiki cha mpingo cha mpingo × 2
Wacha mwenzenu nicheke japo nna pengoo × 2
Waogope wala baata watakuchukua
Kama pesa tutapata mabeibi vumilia
Waogope wala baaata wanaokusumbua
Kama mtonyo tutapaaata
Nasi tutatumia
Wooo wow o woo hiki kisiki cha mpingo cha mpingo × 2
Wacha mwenzenu nicheke japo nna pengoo × 2
Kwa yako madoido hutulii kitandani una fujo
Wamzidi Edi kudo mama wajiweza hadi judooo

Waogope wala baata watakuchukua
Kama pesa tutapata mabeibi vumilia
Waogope wala baaata wanaokusumbua
Kama mtonyo tutapaaata
Nasi tutatumia

***Chanzo: Radio Zanzibar tarehe 15/2/2015***

**Diamond: 3. *Number One***

Wasafi
Kwanza mapenzi safari
Ujana ni maji ya moto walinenaga zamaniii
Pili tumetoka mbali kwa matatizo changamoto
Kwa visa visa fulaaanii
o Tatu kidonda chako kwangu maraadhii
aii Usononekapo kwangu simaanzii
Kwa mahaba ulonipa nimenogewa
Vurugu patashika aa punguza kidoogo
Hapo hapo uliposhika uukiongeza kidoogo
Mi mwenzako taumia number one
My sweety sweety number one
My baby baby number one
My darling number one
Roho yangu mama number one
Na nna wivu sikatai mana uchungu wa mapenzi naujua × 2
So usije kunilaghai kuacha kuzama ukanizingua
Mwenzio naogopa now should me how they do
Aaaaaaa I know
Baby baby number one
My darling number one
Roho yangu mama number one
Na watuache tulaaale

***Chanzo: Radio Zanzibar tarehe 15/2/2015***

**Mwimbaji Diamond: 4. *Kitorondo***

Nimetembea tembea bara na visiwani
Ila nikajionea wewe ndo my number one
Natamani nikupe hela sinaaa
Umejaaliwa upendo heshimaa
Maneno yo matamu sikwibe mama
Wajue binaadamu wabaya sana
Wana wivu hao, haoo haoo
Wachonganishi haoo, haooo haoo
Usijenge chako mnyonge nachechemea
Ata mfinyango na tonge ukalale kwako
Mwendawazimu kaingiaje

Asije kitorondoe
Mwendawazimu kaingiaje
Kitorondo kitorondoe
Mwendawazimu kaingiaje
Ooo kitorondoo
Ingawa nyumba ya shetani
Mwendawazimu kaingiaje
Ukitoka kuta mabinti usinuneee
Nikumbatie unikisi nijivuneee
Kasha zidisha ufanisi jitumeee
Tujenge nyumba hadi uparisi wanunee
Ni michezo michezo ya saluni chunga
Wasije kufunza hadi uhuni ukaganda
Kaanza safari mchana jua kali usiku halali ayaaaa
Wana wivu hao, haoo haoo
Wachonganishi haoo, haooo haoo
Mwendawazimu kaingiaje
Asije kitorondoe
Mwendawazimu kaingiaje
Kitorondo kitorondoe
Mwendawazimu kaingiaje
Ooo kitorondoo
Ingawa nyumba ya shetani
Mwendawazimu kaingiaje
Usijali lawama
Wacha wanizonge
Usiku mchana
Darling nakupenda
Ooo kachiri, kachiri ndo dawa yangu
Mwenzangu ni taabani
Niliondie roho yangu
Wasije wafurahi
Wakaiba tamu yaaangu
Wasafi
Mwendawazimu kaingiaje
Asije kitorondoe
Mwendawazimu kaingiaje
Kitorondo kitorondoe
Mwendawazimu kaingiaje
Ooo kitorondoo
Ingawa nyumba ya shetani
Mwendawazimu kaingiaje

***Chanzo: Radio Zanzibar tarehe 15/2/2015***

**Mwimbaji Barnaba: 5.** ***Mapenzi Shida***

Mapenzi shida pesa ndo kabisa
Nishike wapi najihisi nadhalilika
Waaala delwa × 6
Huku niliko jogoo limewika
Kuku jike ananiumiza na kunipa shida
Ana mtondo goo, jogoo kila siku anataka
Mimi kanisevu anko Ali
Mwengine dalali
Yupi wa halali × 2
Kama shida zangu ni hali
Ungesema za zamani
Kama shida na vitimbwi × 2
Baby so wala delwa
Mapenzi shida pesa ndo kabisa
Nishike wapi najihisi nadhalilika
Waaala delwa × 6
Aaaaaaa baby wa halali
Kama simu ningenunua tochi
Muli mulika nimemulika kwenye kiza
Sijaona mtu kizungu × 2 mkuti
Mwenyewe kanipiga kibuti
Kafanya kusudi
Nishike wapi najihisi nadhalilika
Waaala delwa × 6

***Chanzo: Radio Zanzibar tarehe 15/2/2015***

**Mwimbaji Sultan King: 6.** ***Bado mi Nakuhitaji***

Nna amini Mungu amemshusha duniani
Malaika pekee tanilinda maishani
Uzuri wake hata sijui ufanane na nani
Labda wangu maami × 2
Moyo wangu unaniuma nisipokuona
Naumia na sijui kwa nini
Niamini we pekee ndie nnaae kupenda moyoni
Na nnae kuthamini
Baby halow mwenye sura nzuri yoo
Nnakwita queen baby girl
Jua we ndo wange mchumba
Ndani ya moyo wanguuu eee
Tusijali kuchekwa amini po siku nasi tacheka helow
Wambea sikupe presha wameahidi penzi letu kushusha eeee × 2
Moyo wangu unaniuma nisipokuona
Naumia na sijui kwa nini
Niamini we pekee ndie nnaae kupenda moyoni
Na nnae kuthamini
Baby halow mwenye sura nzuri yoo

Nnakwita queen baby girl
Jua we ndo wange mchumba
Ndani ya moyo wanguuu eee
Baby bado mi nakuhitaji × 2
Bado mi nakuhitaji × 2
Baby halow mwenye sura nzuri yoo
Nnakwita queen baby girl
Jua we ndo wange mchumba
Ndani ya moyo wanguuu eee

***Chanzo: Radio Zanzibar tarehe 15/2/2015***

## KIAMBATISHO: 3

## NYIMBO ZA WATOTO AMBAZO HAZIKUTUMIKA KATIKA UCHAMBUZI WA DATA

### 1. *Hakuna Gogo Pumbavu*

Hakuna gogo pumbavu
Hoya
Lishindalo la mnazi
Hoya
Ukilipiga mashoka
Hoya
Humo ndani liko wazi
Hoya
Kuna wingi wa vitwana
Hoya
Na wingi wa vijakazi
Hoya
Shikeni jembe tulime
Hoya
Uvivu hauna kazi
Hoya
Kipakacha nkumbatire bwana
Naona baridi sana

***Chanzo:Watoto wa mtaa wa Mkunazini Unguja tarehe 16/2/2015***

### *2. Nalia Nalia*

Nalia nalia nalia kisuru Jumbe
Jumbeee Songoro kaiba kunde
Kaiba kundengwa kamsingizia Mra
Mraaae kasema utakwenda ona
Utakwenda ona pingu na mikono nyuma
Nyuumaae na misumari ya chuma
Kazipata hoho mbili kazitia mchuzini
Mtwana Marimba mchuzi una hoho
Ukinipa nautaka tu kwa uroho

***Chanzo:Televisheni Zanzibar tarehe 17/2/2015***

### *3. Watoto Wangu*

Watoto wangu ee
Ee
Mimi mama yenu
Ee
Sina nguvu tena
Ee

Za kuuwa samba
Ee
Samba ni mkali
Ee
Ameuwa baba
Ee
Ameuwa mama
Ee
Haidhuru piteni

***Chanzo:Televisheni Zanzibar tarehe 17/2/2015***

**4. *Watoto Muwangapi***

Watoto muwangapi?
Tuwale waleee saba Mbaraka
Kidenge denge nakuja
Mbaraka
Najachukua wangu
Mbaraka
Twalia lia, twalia lia
Twamlilia Fatuma
Wana mmakondee
Wamemchukua
Wana mmakonde
Wana mmeng'enyuraaa

***Chanzo: Televisheni Zanzibar tarehe 17/2/2015***

***5. Njugu Ni Lembwe***

Njugu nilembweeee
Njugu nileembwe
Alie nyuma
Atangulie mbele
Wausoni tweeende

***Chanzo: Wanafunzi wa Skuli ya Darajani tarehe 18/2/2015***

## KIAMBATISHO: 4

## PICHA MBALIMBALI ZINAZOONESHA WATOTO WAKICHEZA NA KUIMBA



1. ***Wanafunzi wa Skuli ya Darajani Unguja wakiimba wimbo wa Hodi na Karibu, (chanzo mtafiti Skuli ya Darajani 12/2/2015)***



2. ***Watoto wa mtaa wa Mkunazini Unguja wakiimba na kucheza wimbo wa Shuwadina, (chanzo mtafiti Shehia ya Mkunazini Unguja 14/2/2015)***



3. ***Wanafunzi Skuli ya Mkunazini Unguja wakicheza na kuimba wimbo wa Nasaka Mke Wangu, (chanzo mtafiti Skuli ya Mkunazini 13/2/2015)***



*4. Watoto wa mtaa wa mkunazini wakicheza na kuimba wimbo wa Kama Dada Wanipenda, (chanzo mtafiti Shehia ya Mkunazini 14/2/2015)*